NEEMA YA MUNGU IOKOAYO

NEEMA YA MUNGU IOKOAYO

UTANGULIZI:

Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu
wote imefunuliwa" (Tito 2:11).

Katika dunia hii tunayoishi wanadamu wanakabiliwa na maamuzi mbalimbali ya kufanya maishani mwao. Maisha aliyo nayo sasa, na baadaye ni mambo ambayo kila mtu anayafanyia maamuzi, kwamba anafanya kwa kujua au kwa kutokujua. Miongoni mwa maamuzi makubwa sana ambayo kila binadamu anayafanya ni kuhusu mambo ya imani, yaani dini.

Dunia yetu inazo imani au dini kadhaa, ambazo pia zimegawanyika katika madhehebu au vikundi mbalimbali. Jambo hili lazima linasababisha hali ya kuchanganyikiwa kwa watu wengi, kama hali halisi ilivyo hasa ukizingatia kuwa dini hizo zote zinadai kuwa na Mungu mmoja wanayemwabudu. Ni lazima mtu ajiulize swali na kulipatia jibu. Na swali lenyewe ni kwamba, Inawezekana kweli kwa Mungu aliye mmoja, aliyeumba mbingu na nchi na vyote vilivyomo atoe miongozo mbalimbali inayotofautiana na hata kupingana, kwa watu wake anaohitaji wamwabudu yeye peke yake? Na kama Yeye ni mkamilifu na asiyeweza kufanya makosa, kwa nini hali iwe ya kuchanganya mawazo namna hii?

Hivyo basi, ni hakika kuwa lazima kuna udanganyifu unaofanyika katika mambo haya ya dini. Ndiyo sababu kwa Upendo wake usio kifani, Mungu wetu kwa kutambua kuwa hali ya udanganyifu itakuwepo, alitupatia neno lake – yaani Maandiko Matakatifu au Biblia. Maandiko haya yanasema hivi katika Zaburi 119:105, "NENO LAKO NI TAA YA MIGUU YANGU, NA MWANGA WA NJIA YANGU."

Neno la Mungu ni taa ili tusitembee gizani, ni mwanga ili tusije tukaacha njia ya kweli na kufuata njia nyingine za uongo. Hivyo msomaji, Mungu wetu hakutuacha gizani, tulitafute neno lake kwa bidii, na kulisoma na kujitoa kumtii katika kila jambo. Katika kitabu cha 2 Timotheo 3.:15 tunasoma "Na ya kuwa tangu utoto umeyajua Maandiko Matakatifu, ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu kwa imani iliyo katika Kristo Yesu ." Neno la Mungu linahekimisha hata kupata wokovu .

Kwamba wokovu ni nini, na unapatikanaje, ndilo somo Kuu la Kigazeti/kijitabu hiki. Hebu fungua moyo wako ili Roho Mtakatifu akuongoze kuyatambua mapenzi yake na kuyatenda. Kumbuka mambo ya Kiroho hutambulikana kwa jinsi ya rohoni.

Ni ombi la Mtayarishaji.

HISTORIA FUPI YA ANGUKO

Maandiko Matakatifu huelezea hali ya dunia na vyote vilivyomo mara baada ya uumbaji kuwa "Mungu akaona kila kitu alichokifanya, natazama ni chema sana….." (Mwanzo 1.31). Hivyo mwanadamu alikuwa mkamilifu alipotoka mikononi mwa Mungu. Je ukamilifu huu ulitokana na nini? Ulitokana na kipimo kile ambacho Mungu alikuwa akimtazama mwanadamu - Kiwango cha ukamilifu ambacho ni sheria takatifu ya Mungu. Na kwa kadri mtu alivyodumu katika utii huo wa sheria au kanuni za Muumba wake, aliendelea kuwa mkamilifu. Lakini jambo moja lilitokea katika viumbe vya Mungu. Uasi dhidi ya sheria hii takatifu ya Mungu ulitokea Mbinguni, ukianzia kwa yule malaika aliyeitwa Lusifa, na uasi huo ukafika katika dunia yetu hii, pale Adamu na Hawa walipomwamini shetani.

Watu wengi huwa na mtazamo tofauti wanaposikia "Sheria ya Mungu" maana hufikiria juu ya usifanye hiki au kile – ***"usi"*** na hivyo wanafikiria juu ya Kanuni ngumu ambazo Mungu amemwekea mwanadamu ili azifuate. Lakini je, hii sheria ya Mungu hasa ni ipi? Ni ile sheria Kuu ya Upendo. Na ieleweke kuwa upendo huu wa Mungu sio ule tunaoufikiria na kuufahamu. Upendo huu wa kimbingu ni ule amabao umeelezwa kama "AGAPE". Ni Upendo usio na Ubinafsi. Unaweza kuliona na kulitambua hili katika uumbaji – yaani Mungu alipoumba viumbe alikuwa anatoa uhai wake na mema yake yote ili yafurahiwe na wengine, hakutaka kujilimbikizia mwenyewe. 1Yohana 4:8 anasema, "Yeye asiyependa hakumjua Mungu, kwa maana Mungu ni Upendo." Ndio maana Bwana Yesu alipoulizwa kuhusu amri iliyo kuu, alijibu kwa kuonyesha kuwa Upendo Kwa Mungu na kwa mwingine ndio msingi wa amri au sheria (Mathayo 22:36-40). Sheria iliyo ya Uhuru – yaani ya hiari.

Shetani alipoanzisha uasi mbinguni kwa madai kuwa Mungu ameweka Kanuni ngumu kwa viumbe vyake kuzitii, ni kuwa alikuwa anaonyesha kutoweka kwa upendo huo wa Mungu ndani yake, ambako kwa maana halisi ni kutoamini. Upendo ukatoweka moyoni na sasa Ubinafsi ndio ukawa mfumo bora kwake. Na kwa sababu aliona chuki dhidi ya Mungu na sheria yake ya Upendo, kusudi lake likawa kumuua Mungu na wafuasi wake ili aanzishe himaya yake ambayo yeye atakuwa ndiye mkuu (soma Isaya 14:13-14). Na hii ndiyo sababu akaanzisha vita mbinguni (soma Ufunuo 12:7-9). Baada ya shetani kushindwa vita mbinguni alishuka akiwa na ghadhabu nyingi akikusudia kuharibu hali njema ya viumbe na mpango wa Mungu kuhusu uumbaji. Ndipo alipopata nafasi katika dunia yetu hii. Soma pia Ezekiel 28:11-15.

Jaribu Na Anguko

Shetani alimjaribu Hawa pale Bustani ya Edeni, Alijenga jaribu lake katika kumfanya Asimwamini Mungu. Alimfanya Hawa aone kuwa Mungu hana upendo kwao, ana ubinafsi, ndio maana amewazuia au kuwaficha mambo fulani ambayo yangewapatia furaha zaidi; tabia ambayo kwa kweli ni ya shetani mwenyewe. Maana shetani hakuwa na upendo kwa Mungu na viumbe vyake. Angalia alivyomwambia Hawa "Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo Mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya" (Mwanzo 3:45).

Katika maneno haya tunaona Uongo ukichanganywa na ukweli kidogo na kuleta udanganyifu Mkuu kwa Hawa. Ukweli ni kuwa shetani hakumwambia Hawa ukweli. Watu wengi wanaamini kuwa madai ya shetani kwamba Mungu aliwaficha Adamu na Hawa mambo fulani mazuri ni ya kweli. Lakini hebu tuchunguze kidogo ukweli wa madai haya:-

"Hakika hamtakufa." – Katika Mwanzo 2:17b Mungu aliishamwonya Adamu kuwa kama angeasi angekufa, "Utakufa hakika." Kwa hiyo maneno haya ya shetani yalikuwa uongo kabisa (soma Warumi 6:23a). "Mtafumbuliwa Macho." – Katika maelezo haya, Shetani alikuwa akijenga wazo kuwa, pamoja na kwamba walikuwa wanaona, lakini bado walikuwa wamefichwa mambo fulani ambayo ni mazuri na njia pekee ya kuyafahamu na kuyaona ni kwa kumwasi Mungu. Lakini ukweli ni kuwa hakuna jema lolote ambalo Bwana aliwaficha. Kumbuka sheria yake ni ya Upendo usio na Ubinafsi.

“Mtakuwa kama Mungu” – Kufanana na Mungu. Katika Mwanzo 1:26, “Mungu akasema ‘na tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu…..”. Kwa hiyo shetani alijifanya kumweleza Mwanadamu hali bora zaidi ambayo angekuwa nayo kwa kuasi. Lakini hali ya kufanana na Mungu tayari mwanadamu alikuwa nayo. Leo, tunaposema hivi, inakuwa jambo gumu kuingia akilini. Lakini Adamu na Hawa walimwona Mungu, wakaongea naye uso kwa uso, walimjua vizuri, ndiyo maana unapotafakari waliwezaje kufikiri hawafanani na Muumba wao, na sasa walitafuta kufanana naye kwa jinsi ipi, inakuwa vigumu kuelewa. Hali kamili ya kufana na Muumba wetu tuliipoteza kwa kukubaliana na maneno ya shetani. Tulipoteza utukufu wa Mungu (soma Warumi 3:23).

“Mkijua Mema na Mabaya.” Mti wa Ujuzi wa mema na mabaya uliwekwa kuwa kipimo cha upendo wao kwa Mungu, upendo ambao ungedhihirishwa kwa Utii wao kwa Muumba wao. Sasa swali la kujiuliza ni kuwa, je, mwanadamu hakuwa na Ujuzi wa jambo lolote kabla ya kula matunda ya mti Huu? La, alikuwa na Ujuzi wa mema, maana haya yaliumbwa ndani yake (soma Waefeso 2:10) na ndiyo aliyotenda tu hadi siku ile alipoanguka (soma Mwanzo 1:31; 3:2-3).

Kula matunda ya mti huo kuliongeza kitu kigeni – kulifungua mambo mabaya (*maovu*) ambayo mwanadamu hakutegemea ndiyo yangekuwa matokeo ya uasi wao. Na mabaya hayo yanazidi kuzaliana hata leo. Badala ya ujuzi huo kuleta Mema kama shetani alivyowatumainisha, umeleta misiba na mauti, na kumtenga Mwanadamu mbali na Muumba wake. Matumaini aliyowapa yakawa ya uongo. Kutokana na kupandikiza Ubinafsi ndani yao walitegemea kufaidika, kumbe ikawa hasara ya milele.

Kwa njia hii shetani alifanikiwa kumfanya mwanadamu kumtazama Mungu kwa picha nyingine. Badala ya kumuona kama Muumbaji wao anayewapenda na kupenda kuwapatia mema, walimwona Mungu kama Mtawala aliye na ubinafsi na aliyeweka sheria ngumu kwa viumbe vyake ili kuzitii. Na huu ndio mtazamo wa mamilioni ya wanadamu leo kumhusu Mungu. Shetani akafanya Mungu aonekane kwa sura ambayo kwa kweli ni ya Shetani mwenyewe yaani Ubinafsi. Dini hii ikaanzishwa. Muumbaji wetu akawa adui yetu, na shetani aliyekuwa adui akawa rafiki yetu. Ubinafsi huu ndio msingi wa dini au imani zote zisizomkubali Yesu kama njia pekee ya wokovu.

Mara baada ya anguko mwanadamu alipoteza haki zote alizokuwa amepewa na Mungu. (Kumbuka kuwa uumbaji lilikuwa ni tendo la Mungu la Upendo, alilolifanya kwa hiari yake mwenyewe, na viumbe vyote ili vifurahie uumbaji wao vilipaswa kuishi kwa kanuni ambazo ziliwekwa na Muumbaji wao). Haki ya mwanadamu saa hiyo ilikuwa ni kufa palepale, maana alikuwa amejiondoa chini yake aliye asili ya uhai au uzima. Kwa hiyo Mungu alikuwa na haki kabisa ya kuchukua dunia yake na viumbe wengine wote aliowaweka chini ya mamlaka ya Adamu na kuviondoa, Je mwanadamu angeelea angani? Lakini, anga pia ni la Mungu. Kadhalika Muumbaji alikuwa na haki ya kuchukua pumzi yake ya uhai na mwanadamu kurudia udongo tena. Ni hakika kwa tendo la Ubinafsi ambalo mwanadamu alitegemea kujipatia zaidi, sasa alipoteza vyote.

Matokeo ya Uasi yalikuwa Nini?

Mwanadamu alipoteza utukufu wa Mungu (soma Mwanzo 2:25; 3:7; Rumi 3:23).

Alipoteza haki ya kuwa hai (uzima wa sasa na wa milele) (soma Mwanzo 2:17).

Alijifanya kuwa adui wa Mungu (soma Mwanzo 3:8).

Alipoteza uwezo wa kutii sheria za Mungu (soma Zaburi 14:23).

Katika hali hii mwanadamu alipoteza uhusiano na Mungu – Ndipo Biblia inasema “Toka Mbinguni Bwana aliwachungulia wanadamu, Aone kama yuko mtu mwenye akili, amtafutaye Mungu. Wote wamepotoka, wameoza wote pamoja. Hakuna atendaye mema, La! Hata mmoja,” (Zaburi 14:23).

“-------Hakuna mwenye haki hata mmoja. Hakuna afahamuye, Hakuna amtafutaye Mungu.” (Warumi 3:10-11). Katika Isaya sura halisi ya uasi imefananishwa na mgonjwa ambaye labda, kamwe hujawahi kukutana naye au kumwona, inasema “---------Kichwa chote ni kigonjwa, moyo

wote umezimia. Tangu wayo wa mguu hata kichwani hamna uzima ndani yake; bali jeraha na machubuko na vidonda vitokavyo usaha; havikufungwa, havikuzongwazongwa, wala havikulainishwa kwa mafuta," (Isaya 1:5-6).

Je, mtu wa Mungu unajua hivi ndivyo tunavyoonekana katika hali yetu ya uasi na darubini ya Mbinguni? Je mgonjwa wa jinsi hii atawezaje kujiokoa au kujiponya mwenyewe? Hata kama angetaka kufanya, kumbuka neno la Mungu linasema "tangu wayo wa mguu hata kichwani hamna uzima ndani yake" – amekufa. Hakika hakuna njia ya kujinasua wenyewe katika hali hii. Hii ndiyo hali yetu pasipo Kristo. Tafakari kwa Makini.

Mungu Aingilia Kati

Sheria takatifu ya Mungu iliyovunjwa ilidai uhai wa yule Mhalifu (soma Mwanzo 2:17). Lakini kwa Upendo Mkuu wa ajabu, Mungu aliandaa mpango wa pekee utakaompatia mwanadamu nafasi nyingine ili kuweza kuishi kwa kanuni hii ya Kimbingu yaani Upendo usio na Ubinafsi. Mpango huo ndio unaoitwa Mpango wa Wokovu (soma Zaburi 111:9).

Mpango wa Wokovu

Mungu alitangaza kwa mwanadamu na nyoka juu ya kile atakachokifanya kati yao. Kumbuka baada ya uasi mtu akawa adui wa Mungu na rafiki ya shetani. Mpango huu wa wokovu ambao ni wa Mungu mwenyewe ulifanya kitu. Mwanzo 3:15 inasema, "Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake, huo utakuponda kichwa na wewe utamponda kisigino." Mungu akavunja urafiki kati ya Mwanadamu na Shetani kwa kuweka uadui – na hicho alichofanya ndiyo "Neema." Wengi wameelekeza zaidi mawazo yao kwa hawa nyoka wa kawaida na kumsahau Shetani mwenyewe ambaye ndiye adui hasa (soma Ufunuo 12:7-12, 17).

Mungu wetu akijua kile ambacho kingetokea, aliandaa mpango wa wokovu tangu Mwanzo. Katika Ufunuo 13:8b tunasoma, "------Mwanakondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia". Soma pia 1 Petro 1:18-20. Ni kwa sababu Bwana Yesu alikuwa amekwishajitoa kuwa "mwanakondoo wa Mungu achukuaye dhambi za ulimwengu" ndio maana Adamu na Hawa hawakufa mara tu walipokuwa wamekula matunda ambayo Mungu aliwakataza wasile. Lakini pia wanadamu tumeendelea kujiuliza swali moja kubwa kuhusu jambo hili na mara nyingine majibu labda yameonekana kutotosheleza mashaka ya mwanadamu.

Lakini kama tukitafakari kwa makini ukweli wenyewe tutaridhika. Swali lenyewe ni hili "Kama Mungu alijua yote yatakayotokea, kwa nini hakuyazuia? Na kwa nini hakumwangamiza shetani mara tu alipoasi ili asiambukize uasi wake kwa viumbe wengine?

Jibu ni kuwa Mungu ni <u>Upendo</u>, na upendo unaandamana daima na haki (yaani kutenda haki). Je, hatua za kuzuia uasi zilifanyika? Ndiyo. Kwanza kwa kufundisha viumbe vyote juu ya kanuni hii kuu ya kimbingu yaani <u>Upendo</u>. Hivyo viumbe vilipaswa kuishi kwa kanuni hiyo tu ili kudumisha furaha ya ulimwengu. Lakini pia shetani alipoanzisha uasi rasmi, Mungu alimwonyesha wazi matokeo yake, na kumsihi aachane na mipango yake iliyokuwa kinyume, lakini hakukubali. PP - Chapter isemayo 'why was Sin permitted'?

Kwa nini asimharibu shetani mara moja? Tafakari kwa makini unajua Mungu wetu **alishitakiwa** na shetani kwa viumbe wake kuwa - Yeye si mwenye haki. Hakutoa uhuru ili wao (viumbe) waishi kama wapendavyo. Yaani ni mtawala asiyewapenda na asiyependa furaha yao. Kama Mungu angemwangamiza shetani palepale. Hakika shetani angeonekana kuwa mkweli, na ile kanuni ya **Upendo usio na Ubinafsi** ingekuwa imevunjwa na Mungu mwenyewe. Lakini kwa kuwa Mungu ni upendo na yeye habadiliki ndio maana ilibidi ushahidi udhihirike wazi kwa viumbe wote kuwa ni nani hasa aliye mwema - Mungu au shetani? Kumbuka daima **haki ina gharama.**

Kwa hiyo ili Mungu audhihirishe upendo wake na haki yake - dhambi imemgharimu sana kuliko tunavyoweza kufikiri. Ili hatimaye viumbe wenyewe waamue na kukiri kuwa - Hakika Mungu wetu ndiye mwenye haki. Kumbuka mashitaka yoyote yanahitaji ushahidi, hivyo mshitaki aeleze mashitaka yake yasikilizwe na kupimwa. Na mshitakiwa naye aeleze ukweli usikilizwe na kupimwa. Sasa tafakari maelezo machache yafuatayo:-

1. Malaika waliishafanya uamuzi juu ya ukweli kuhusiana na mashitaka haya. Theluthi ya malaika waliamua kuungana na Shetani (soma Ufunuo 12:3-4). Theluthi mbili walidumisha utii kwa Mungu.

2. Sayari nyingine ambazo hazikuasi zilikwisha fanya uamuzi, na kudumu kuwa upande wa Muumba wetu (soma Ufunuo 12:10-12)a.

3. Dunia yetu ilimkubali shetani na kanuni zake za **Ubinafsi,** lakini Mungu wetu kwa Upendo aliingilia kati ili **kutuokoa**. Unajua kwa nini hadi leo vita hii haijafikia mwisho wake? Ni kwa sababu wanadamu tumeendelea kudumu katika njia panda kwa mda mrefu. Wapo waliokwisha kuchagua kuwa upande wa Mungu (wachache), wapo wameamua kuwa upande wa Shetani, na wengi sana hawajajua la kufanya. Ukweli ni kwamba, ijapokuwa wanadamu wengi wanadai kuwa na imani kwa Mungu kwa madai kwamba wana dini, lakini imani ya kweli haiko wazi kwa mamilioni ya watu. Yawezekana ukawa mmoja wao!! Kwa hiyo ndiyo maana Mungu anatusubiri tufanye uamuzi huo. Lakini ni lazima watu waamue kwa kufahamu wazi ni nini wanachofanya. Ndiyo maana Bwana Yesu, baada ya kueleza dalili nyingine zitakazoonyesha mwisho wa dunia, akasema "Tena habari njema ya Ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote, hapo ndipo ule mwisho utakapokuja" (Mathayo 24:14)

Je, mpendwa unajua kuwa mahubiri mengi sana ambayo yamekuwa yakifanyika hayajahubiri hii "**habari njema ya Ufalme**" kwa nuru yake halisi? Na je, wewe binafsi unafahamu hiyo habari njema ni ipi? Napenda kukujulisha kuwa hili ndilo somo kuu la maandiko haya. Unapokuwa ukiendelea kujifunza, hebu uwe mwenye maombi ya kweli na makini ili kujifunza, kuelewa, kuupokea na kuuishi ukweli huu wa pekee, Mungu akubariki, anakusubiri ufanye uchaguzi sasa na si baadaye - ili vita kuu ifike mwisho (soma 2 Kor. 6:2).

KRISTO HAKI YETU

Mungu ashukuriwe kwa kumtoa Bwana Yesu kwa ajili yetu. Unapoendelea kujifunza mpango huu wa ukombozi daima zingatia maneno haya **"Kristo haki yetu."** Kile ambacho Wanadamu tulipoteza katika Adamu, Mungu wetu amekirudisha katika Kristo Yesu. Ndiyo maana mpango huu kwa hakika ni wa kumrudisha mwanadumu katika hali ile aliyokuwa nayo kabla ya kuanguka dhambini. Sasa swali - Kristo anakuwaje haki yetu? Kumbuka kuwa mara baada ya uasi, mwanadamu alikuwa amejitenga kabisa na Mungu, lakini Mungu ndiye asili ya vyote, kwa hiyo mtu hakuwa tena na haki ya kutumia chochote kilicho cha Mungu - tangu pumzi ya uhai, chakula, mwanga wa jua, dunia yenyewe, maji na kila kitu unachoweza kukifikiria. Mwisho wake ulikuwa ni kifo tu, tena cha milele, maana angewezaje kuupata tena uhai na yeye alipewa tu na Mungu? Ndiyo maana katika Biblia Yesu anasema, "---- Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele" (Yohana 10:10). Ni kwa sababu ya kafara ya Kristo ndio maana tuna uzima huu wa sasa (uzima) na kisha kuna ahadi ya uzima tele (wa milele) katika ufalme wake ujao. Kwa hiyo vyote tunavyopata ili kutusaidia sasa kwa maisha haya vimenunuliwa kwa damu ya Yesu ya thamani - yaani hewa tunayovuta, nuru ya jua, mvua, maji, chakula na vingine vyote. Unapolitambua hilo, ndipo hutakuwa mharibifu au mtumiaji mbaya asiyejali vitu hivyo. Kwa hiyo kama isingekuwa Kristo Yesu, wanadamu wote tusingekuwepo. Tunaishi leo kwa kuwa yeye **- Yesu - ametununulia haki hiyo**. Na kwa vile mauti ilikuwa ya milele, pia kwa kafara yake ametu-nunulia uzima wa milele. Kwa hiyo utaona kuwa mwanadamu hana chochote anachoweza kukidai kuwa kingempatia haki ya kuishi, isipokuwa tu-kile alichofanya Mungu wetu kupitia kwa Yesu Kristo Bwana na Mwokozi wetu. Ni haki ya Kristo tu inayotupatia vitu vyote. Ndio maana yeye ni haki yetu. Je, ulifahamu hayo? Au ni kitu kipya? Na je, watu wengine wanafahamu hivyo? Je, unajua kuwa katika Kristo Yesu, tuna haki ya kuishi sasa, na

hatimaye milele siku ile ajapo? Hii ndiyo habari njema. Je umeielewa vizuri na kuipokea? Kwa sababu habari hii ndiyo "Injili" yenyewe, hakika tunahitaji kuifahamu vizuri ili kuipokea au kuikataa. Na kwa kuwa hakuna ukweli mwingine zaidi ya huo, kumbe ni ujumbe muhimu sana kwa maisha yetu. Hebu tafakari fungu lifuatalo:-

> "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda Ulimwengu, hata akamtoa mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele". Yohana 3:16.

Mungu wetu **alipenda** na **kutoa**. Sisi tunachotakiwa kufanya ni kuamini tu. Kama ujumbe ndiyo huu, mbona inaonekana kuwa Wakristo, ambao ni wengi duniani, wamekuwa wakidai wanauamini na kuuhubiri, na bado inaelekea mwisho hauji? Endelea kujifunza na nuru zaidi itakuangazia.

Jambo la muhimu ni kwamba, kama "habari njema ya ufalme" itaeleweka vizuri na kupokelewa, au kama watu wote wataamua kuhukumu kesi hii ambayo Mungu ameshitakiwa, kwa kujiweka upande wa Mungu au Shetani - dunia hii itashuhudia mabadiliko makubwa ambayo hayajawahi kuwepo tangu dunia kuwepo, na ndipo mwisho utakapokuja. Sasa swali jingine ni hili - Je, tunawezaje kuupokea ukweli huu ili uwe halisi maishani? Neno la Mungu linasema ni kwa njia ya **Imani** - Yohana 3:16. Ndipo tunapoingia katika hatua nyingine ya somo hili. Unajua kwa nini maisha ya kumcha Mungu yanaonekana kuwa ni maisha magumu (yaani ni mzigo) kwa watu wengi? Ni kwa sababu hatujamfahamu Yesu na kumpokea kama haki yetu - Habari njema. Watu wengi sana wanajaribu kumfanya Mungu awapende kwa kujitahidi kutenda mema. Lakini neno la Mungu linasema yeye hajawahi kutuchukia hata wakati mmoja - yaani siku zote anatupenda. Wengi tunajaribu kumpenda Mungu ili atusamehe dhambi na halafu atupatie uzima wa milele, asitutupe jehenamu. Lakini unajua haya yote **Mungu amekwishayafanya** kwa **ajili ya watu wote katika Kristo? Yaani, Kwa njia ya Kristo Yesu, wanadamu wote tumesamehewa dhambi** (**Kupatanishwa na Mungu**) na hivyo uzima wa milele ni matokeo ambayo hayana budi kutokea kwa kila atakayekubali **kuamini** ukweli huu. Na ndipo maisha ya kumfuata Kristo yatakuwa furaha tupu - iwe ni katika raha au shida. Biblia itadhihirisha ukweli huu. Ndiyo maana injili ni habari njema. Haiwezi kuwa njema halafu hapo hapo iwe mbaya au mzigo. **Kumbuka**: Ukiona dalili ya uumini kuwa mzigo au adhabu maishani, basi umeanza mahali pasipo sahihi. Tafuta uanze upya, maana vinginevyo hutafika pale ulipokusudia. Lakini kwa bahati mbaya sana, wengi tunaosema ni Wakristo, hiyo ndiyo hali yetu. Endelea kujifunza ili uwe na amani ya Yesu moyoni. Ni heri kwetu kama tutaanza upya kwa usahihi kuliko kuendelea na kile tunachodhani pia ni sawa tu - kisitufae.

INJILI KATIKA AGANO LA KALE:

Watu wengi sana huamini kuwa kipindi cha agano la kale watu walikubalika mbele za Mungu kwa kuzishika sheria, na kipindi baada ya kuja Kristo sasa tunakubaliwa kwa **neema**. Lakini, je, umewahi kujiuliza kuwa kama watu waliokolewa kwa kuzishika sheria, wale wanyama waliotolewa kafara walikuwa wa kazi gani? Je, Mungu alikuwa anajaribu mpango ambao anajua wazi hauwezekani? Je, ni kweli huu ulikuwa ndio mpango wa Mungu? La, hasha. Kwa sababu Shetani anafahamu vizuri nguvu ya watu kuipokea injili, yaani habari njema, basi tangu mwanzo alianzisha mfumo ulio tofauti kabisa na mpango wa Mungu, lakini ulioigizwa na kuonekana kama ndio mpango wa Mungu. Hebu sasa tuingie kwa undani zaidi kuona ukweli huu.

ADAMU: Kumbuka, Mungu aliweka uadui kati ya mtu na Shetani (soma Mwanzo 3:15). Baada ya kutangaza mpango huo ambao kwa kweli bila Yeye (Mungu) Adamu hakuwa na mpango wowote wa kumrudia, Bwana alimfundisha Adamu somo la kwanza kabisa jinsi atakavyoonyesha **Imani** yake kwa kile ambacho Mungu alikifanya kwa ajili yake. Mungu alimfundisha ibada ya kutoa kafara.

Adamu alitetemeka kwa hofu kuu kuona akitoa uhai wa mnyama asiye na hatia badala yake, uhai ambao ni Mungu pekee awezaye kuutoa, aliona ubaya wa dhambi kwa sura tofauti kabisa kuliko kabla ya hapo, kama ambavyo dhambi itaonekana kwa yeyote anayemtazama mwanakondoo wa Mungu pale Msalabani. Adamu alipoelezwa kwa upana mpango wa kumwokoa, jinsi ambavyo kwa dhambi yake inabidi mwana pekee wa Mungu ashuke, atwae ubinadamu, azaliwe, ateswe na mwisho kufa

msalabani, alisikitika kwa huzuni ya ajabu. Ndipo akaomba kuwa yeye (Adamu) pamoja na uzao wake walipe gharama hiyo badala ya Mwana wa Mungu. Lakini alielezwa kuwa asingeweza kulipia gharama hiyo, Malaika nao walipoelezwa mpango huo, wakajitoa ili kufa kwa ajili ya mwanadamu badala ya Bwana wao wanayempenda sana, lakini nao pia waliambiwa hawawezi kulipa gharama ya ukombozi. Kwa nini wasiweze?

1 Ni kwa sababu sheria ya Mungu iliyovunjwa ni takatifu sana kuliko kiumbe chochote, maana ndiyo tabia ya Mungu mwenyewe. Hivyo ni yule aliye sawa na Baba, ambaye pia alishiriki katika uumbaji, ndiye tu angeweza kutosheleza matakwa ya sheria ya Mungu iliyo takatifu sana, soma - PP - Chapter - the Plan of Redemption.

2 Mwanadamu alikuwa amepoteza utukufu wa Mungu - hivyo lazima aupate kutoka kwa yule aliye asili ya utukufu - yaani Mungu Mwenyezi.

3 Mwanadumu alipoteza uzima na kiumbe yoyote hana asili ya uhai, isipokuwa Mungu Mwenyewe, yeye ndiye mtoaji (mpaji). Ndiyo maana ilibidi Bwana Yesu aliye sawa na Baba alipe gharama ya ukombozi wetu. Adamu na Hawa waliipokea injili hii iliyohubiriwa kwao, na walionyesha imani yao katika Kristo kwa ibada ya kafara ya wanyama kama Mungu alivyowafundisha. Nao pia wakawafundisha watoto wao mpango huo wa wokovu na ibada kuhusu mpango huo.

Kaini na Habili

Watoto hawa wawili wa Adamu walifundishwa kumwabudu Mungu na pia ibada hiyo ifanyikeje, na maana ya ibada hiyo. Biblia inaonyesha ibada za hawa vijana wawili katika Mwanzo 4:3-5: “Ikawa hatimaye Kaini akaleta mazao ya ardhi, sadaka kwa Bwana, Habili naye akaleta wazao wa kwanza wa wanyama wake na sehemu zilizonona za wanyama, Bwana akamtakabali Habili na sadaka yake, bali Kaini hakumtakabali, wala sadaka yake, Kaini akaghadhibika sana, uso wake ukakunjamana”. Biblia haisemi hili lilikuwa tukio la ngapi la ibada, lakini inaonyesha tofauti ya pekee iliyojitokeza na matokeo yake. Pia ieleweke kuwa tukio hili ni tofauti kabisa na utoaji wetu wa sadaka leo ambapo mtu hutoa kile alichonacho. Ili ionekane kwa nini sadaka ya Kaini isikubaliwe wakati yeye kama mkulima alitoa kile alichokuwa nacho, zingatia kuwa hii ilikuwa ibada maalum ya kutoa kafara ambayo kwa hiyo walionyesha imani kwa mwanakondoo wa Mungu achukuaye dhambi za ulimwengu. Kwa hiyo ilikuwa lazima kiwakilishi halisi kitumike bila kubadilisha. Na ieleweke kuwa hata leo tutakuwa tunafanya ibada kama ya Kaini, kama katika mahali mbingu zilipoweka kitu maalum kutumika kwa ibada, Tutaweka kitu kingine tofauti. Hakitawakilisha kile kilichokusudiwa na Mungu na hivyo tutakuwa tunaonyesha kukosa imani kwa Mungu - kutoamini.

Sasa katika ibada hii ya Kaini ndiyo tunapoanza kuona hasa kanuni za Babeli zikitenda kazi. Shetani akaweka injili nyingine (bandia) badala ya ile ya kweli, Injili ya kweli inasimama katika msingi huu-wokovu ni katika Kristo Yesu kwa njia ya imani; wakati ile injili bandia ina msingi huu - wokovu unapatikana kwa imani na matendo - yaani ni kitu mtu anachopata kutokana na juhudi zake mwenyewe na pale anaposhindwa, basi Mungu anafanya. Na injili hii bandia imeshika mateka wanadamu wengi sana - tangu wale wanaojiita wakristo wa madhehebu yote na dini zote nyingine duniani - Uislamu, Hinduism, Buddha, n.k. Ndiyo maana injili ya kweli ya milele, ile iliyotangazwa na Mungu mwenyewe pale Edeni inahitajika ifahamike katika nuru yake halisi - halafu kila mtu aamue kumpokea Yesu kama tumaini lake pekee la wokovu au kumkataa; na ndipo kila mtu atakapokuwa amekwishafanya uamuzi, Yesu aendelee kusubiri nini? Hapo ndipo ule mwisho utakapokuja. Nuru hii imefunuliwa kwa namna ya peke katika Kanisa la Mungu la Masalio. Lakini wengi sana miongoni mwetu hatujaifahamu na kuipokea, halafu kuipeleke kwa ulimwengu. Je, tutaendelea kuipuuzia hata lini? Mauaji yanayoendelea kuikumba dunia, vita, magonjwa na misiba

mingine mingi inatusonda kidole watu wa Mungu kuwa tunaendelea kuchelewesha ule mwisho. Unapotafakari mambo haya mazito hebu liwe ombi letu kuwa Bwana atusaidie kuufahamu ukweli huu, kuuamini na kuuishi ili kazi yake imalizike na aje kukomesha mateso ya watu na ya viumbe wengine yaliyosababishwa na dhambi.

Kumbuka Habili alikwenda mbele ya Mungu akionyesha imani kwa kile Mungu alichofanya kwa ajili yake, na Kaini alionyesha kutoamini mpango wa Mungu na akaenda na mpango wake mwenyewe wa kazi za mikono yake - yaani matendo, kumbuka mpango huu wa wokovu ni wa Mungu mwenyewe hivyo ili tuokolewe, inatupasa kufuata kile alichosema Mungu kwa usahihi.

Ibrahimu:

Anajulikana kama "Baba wa imani". Mara Bwana Mungu alipomwita atoke katika nchi ya kwao aende katika nchi ambayo yeye Bwana atamwonyesha, Ibrahimu aliondoka bila swali kuwa nchi anayoiendea ikoje, watu wake wakoje, ina rutuba, au ni jangwa, bali alimwamini yeye aliyemwita(soma Mwanzo 12:1-7). Bwana akampa Ibrahimu ahadi nyingine, "Akamleta nje, akasema, tazama sasa mbinguni, kazihesabu nyota, kama ukiweza kuzihesabu, Akamwambia, ndivyo utakavyokuwa uzao wako. Akamwamini Bwana, naye akamhesabia jambo hili kuwa haki" (Mwanzo 15:5-6). Mungu akaendelea kufanya agano na kumpa Abrahamu ahadi zaidi (soma Mwanzo 15:8-21). Zingatia: Kitu alichotakiwa akifanye ni "kulishika agano la Bwana" (Mwanzo 17:9), yaani katika maelezo yote utagundua kuwa Mungu anaahidi atakachomfanyia Abrahamu na wala si Abrahamu atamfanyia Mungu nini. Ibrahimu hakutoa ahadi yoyote, isipokuwa alipokea daima kile Mungu alichokuwa akimfanyia, na ndiyo maana alifikia uhusiano wa juu sana na Mungu, kiasi cha kuwa tayari kumtoa mwanawe pekee - Isaka - kuwa sadaka ya kuteketeza kwa Bwana. Unajua wengi sana tunakosea tunapotafuta uhusiano na Mungu kwa kujaribu kushika sheria fulani, kwa kweli hilo haliwezekani. Uhusiano wa kweli kati yetu na Mungu, utatokana na kupokea kwa imani kile ambacho Mungu ametufanyia. Kumbuka Adamu na Hawa walijificha walipomsikia Bwana bustanini, je wewe na mimi tunaweza kufanya zaidi ya hayo? Soma Warumi 4:1-22 na utafakari kwa makini jinsi Mungu alivyomhesabia haki Ibrahimu. Ni kwa imani tu, wala si kwa imani na matendo. Je unaona mashaka kuhusu ukweli huo? Endelea kujifunza kwa makini. Imani kwa Mungu hongoza kwenye utii. Imani ni sawa na mtu na matendo (utii) ni matokeo ya imani.

Ismaili na Isaka (Maagano Mawili)

Hawa walikuwa ni watoto wa Ibrahimu. Mmoja alizaliwa kwa mjakazi na mwingine kwa mke halali. Wa mjakazi alizaliwa kwa mwili - yaani ni kwa mpango wa Ibrahimu mwenyewe na wa pili alizaliwa kwa ahadi. Katika wana hawa wa Ibrahimu, kuna somo kubwa sana la imani. Ismaili, aliyekuwa mtoto wa mjakazi, alizaliwa kutokana na kutoamini. Kumbuka, Mungu aliishamwahidi Ibrahimu kuwa atampatia uzao mwingi (soma Mwanzo 12:2-7; 15:4-6, 13-16, 18). Lakini mashaka yao kwa Mungu yalifanya atafute njia yake mwenyewe ya kupata mtoto. Kama ilivyokuwa kwa Adamu, ndivyo ilivyokuwa kwa Ibrahimu. Sara mkewe, akamshawishi atende kinyume na mpango wa Mungu. Kwa hiyo Ismaili ni mfano wa kazi ya mtu mwenyewe - yaani imani na matendo. Na Isaka ni kielelezo cha haki ipatikanayo kwa imani - haki ile itakayo kwa Mungu. Ismaili ni mfano wa agano la kale (haki kwa matendo) na Isaka ni mfano wa agano jipya au agano la milele (haki kwa imani) (soma Wagalatia 4:21-31). Sasa shida ilitokea baada ya kuzaliwa mtoto wa ahadi, maana sasa wako wawili, je ni yupi mrithi? Mwanzo 21:8-12 inasema, "Mtoto akakua, akaachishwa kunyonya, Ibrahimu akafanya karamu kuu siku ile Isaka alipoachishwa kunyonya. Sara akamwona yule mwana wa Hajiri Mmisri (Ismaili) ambaye alimzalia Ibrahimu, anafanya dhihaka. Kwa hiyo Sara akamwambia Ibrahimu, mfukuze mjakazi huyu na mwanawe, maana mwana wa mjakazi hatarithi pamoja na mwanangu, Isaka. Na neno hilo lilikuwa baya sana machoni pa Ibrahimu, kwa ajili ya mwanawe. Mungu akamwambia Ibrahimu, Neno hili lisiwe baya machoni pako, kwa ajili ya huyo mwana, na huyo mjakazi wako. Kila akuambiacho Sara, sikiza sauti yake, kwa maana katika Isaka uzao wako utaitwa". Katika kisa hiki kuna mambo kadhaa ya kujifunza:

1. “Mtoto kukua na kufanyiwa dhihaka.” - Unajua, daima katika maisha yetu ya kiroho, ile haki binafsi yaani ya matendo, siku zote hudhihaki ile haki ipatikanayo kwa imani. Yaani tunajisifia haki yetu wenyewe badala ya haki ya Mungu iliyo katika Kristo Yesu kwa njia ya imani (soma Luka 18:9-14). Ndani yetu kila mmoja, haki hizi mbili hushindana daima, na mtu binafsi ndiye ataamua ni haki ipi ishinde. Ndiyo, maana Nafsi ndiye adui mkubwa tuliye naye wa kwanza tunayepaswa kumshinda (soma Mathayo 10:38-39; 16:24-25, Luka 9:23).

2. “Sara akamwambia Ibrahimu, mfukuzemjakazi huyu na mwanawe.” - Hapa tunapata somo jingine tena. Kama neno la Mungu linavyosema, Sara ndiye aliyemshawishi Ibrahimu ili apate mtoto kwa Hajiri. Kwa hiyo, yeye mwenyewe (Sara) lazima afanye toba kwa kosa alilofanya. Ndiyo maana ilibidi yeye ndiye aanzishe mpango huo kati yake na mumewe. Katika maisha yetu leo, kila mtu anayo haki yake binafsi aliyojifanyia, na hakuna mtu mwingine atakayefanya toba kwa ajili ya mwingine ili kuiondoa hiyo haki bandia. Lazima kila mtu afanye kazi hiyo yeye mwenyewe (soma Luka 9:23).

3. “Hatarithi pamoja na mwanangu.” - Kumbuka Ismaili na Isaka ni mfano wa haki mbili tofauti - ile ya Mungu na nyingine ya mwanadamu. Sasa, Katika kurithi ufalme wa Mungu, kwa kweli ni haki ya Mungu tu, itakayotupatia urithi, na wala si haki yetu binafsi. Wala sio haki ya Mungu pamoja na haki ya mwanadamu. Zingatia sana maneno haya usije ukajuta baadaye (soma Warumi 8:28-30, Mathayo 25:34, 37, 46). Kristo ndiye haki yetu pekee ya kuokolewa.

4. “Neno hilo likawa baya sana machoni pa Ibrahimu.” - Kila mmoja wetu anaweza kulishuhudia jambo hili maishani mwake. Yaani matendo yetu yote mema tunayotenda hayawezi kutupatia urithi!! Hakuna lolote la kujisifia! Jambo hilo daima katika utu wetu wa asili ni baya sana machoni petu. Nafsi, nafsi, nafsi, hutafuta kujiinua. Ndiyo maana hata kuiamini “habari njema ya ufalme” huwa ni shida sana. Nafsi hairidhiki kumpatia mwingine sifa zote. Hivyo lazima kitu kifanyike dhidi ya nafsi (haki binafsi), na hicho ndicho neno lifuatalo (soma Mathayo 16:24, Luka 14:26) - KUJIKANA NAFSI.

5. “Mfukuze mjakazi na mwanawe,” (Wagalatia 4:30). - Lazima haki binafsi ifukuzwe, vinginevyo hakuna kurithi. Itafukuzwa kwa njia gani? Kwa kuisulubisha nafsi daima (soma Marko 8:34), maana nafsi daima hushindana na haki ya Mungu (roho) (soma Wagalatia 5:16.17).

Maagano Mawili: Isaka na Ismaili ni mfano wa Maagano Mawili - moja la Sinai na jingine la Yerusalemu wa juu. Ieleweke kuwa maagano haya si yale ya vitabu vya Biblia - yaani kipindi kabla na baada ya kuzaliwa Kristo, Maagano haya ni:

- Agano la Mungu kwa Wanadamu, yaani kile Mungu alichoahidi kutufanyia. Na agano hili ndilo linaitwa “Agano la Milele” au “Agano jipya” (soma Waebrania 8:8.10). Katika Kristo Yesu (soma Zaburi 111:9).

- Agano la mwanadamu kuahidi kile atakachomfanyia Mungu. Nalo huitwa “Agano la Kale” (soma Waebrania 8:9). Agano hili limeelezwa katika ahadi ambayo Waisraeli waliahidi kufanya yote Mungu aliyosema (soma Kutoka 19:8). Lakini unaposoma Biblia, utaona wazi kuwa Israeli hawakuweza kufanya kile walichoahidi. Na pia ieleweke kuwa ni hapa katika ahadi hii ambapo torati inasema “Ayatendaye hayo ataishi kwa hayo,” (Wagalatia 3:12, soma pia Walawi 18:5).

- Kama tulivyokwisha kuona, kutokana na matokeo ya uasi, kwa kweli hakuna mwanadamu anayeweza kutosheleza madai au matakwa ya sheria ya Mungu (soma Waefeso 2:8-9). Wanadamu wengi sana tunasumbuka katika utumwa huu ambao kwa kweli tunamhitaji Kristo ili atuokoe nao. Hebu kumbuka ni mara ngapi umahidi kumfanyia Bwana mambo fulani, iwe ni kwa siri moyoni mwako, kwa kuinua mkono kanisani, kwa kusimama wito unapotolewa au katika nyimbo nyingi tunazoimba kanisani, halafu angalia umeyatimiza kwa uaminifu kiasi gani. Ni hakika, mengi kabisa hatujayatimiza kulingana na ahadi zetu kwa Bwana. Matokeo yake unayajua? Ni yale kuona kuwa Ukristo ni mgumu sana, ni mzigo mzito Mungu aliotupatia kuubeba, na matokeo yake ni kumwona Mungu kama mkandamizaji anayetaka tufanye mambo magumu tusiyoyaweza (soma Wagalatia 4:24). Na hivyo wengi hatuna amani na Mungu,

Mwisho wake ni kukata tamaa na kusema, “Bwana anawajua walio wake, na kama mimi ni wake ataniokoa tu kwa njia yoyote ile, na kama mimi si wake basi hata nikijitahidi vipi bado siwezi kuokolewa”. Na kwa jinsi hii wengi tunamchukia sana Mungu kiasi kuwa kama tungepata nafasi, na sisi tutamsulubisha msalabani. Njia pekee itakayotupatia amani ni kuikubali haki ya Mungu, agano lake kwetu (soma Warumi 5:1).

KUHESABIWA HAKI (HAKI KWA IMANI)

Haki ni nini? Ni kutenda haki (mema) au utakatifu. Je, mtu yeyote anaweza kuitenda iliyo haki? La, hasha maana ndani yetu sisi, hakuna lililo jema (soma Warumi 7:14-19). Mti mbaya unawezaje kuzaa matunda mazuri, (Mathayo 12:34)?

Nini maana ya kuhesabiwa? Kuhesabiwa ni kupewa kitu bila kukifanyia kazi au bila kustahili. Hivyo, kuhesabiwa haki au utakatifu ni kupewa haki hiyo sisi tulio wadhambi. Yaani badala ya kuhesabiwa kuwa wadhambi tunahesabiwa kuwa watakatifu. Je, jambo hili linawezekana kabla ya sisi kushika amri za Mungu? Ndiyo na ndivyo ilivyo maana ndani yetu hakuna jema. Haki hii tunayopewa bure ni ya nani? (soma Isaya 52:3). Isaya 45:24.25 inasema, “---- kwa Bwana peke yake, iko haki na nguvu-----. Katika Bwana wazao wote wa Israeli watapewa haki, na kutukuka”. Tulitangulia kuona kuwa Kristo ndiyo haki yetu. Sasa swali kubwa ni kuwa ni kwa jinsi gani haki (utakatifu) ya Kristo unakuwa wetu? Neno la Mungu linasema ni pale tunapomwamini Yesu kama Bwana na mwokozi wetu (soma Warumi 3:23-24). Ni wakati gani Mbingu zinapomhesabu mtu kuwa amemwamini Yesu? Ni pale mtu anapoona utakatifu wa sheria ya Mungu kwa kuona na kutambua gharama iliyolipwa msalabani; akaona na kutambua ubaya wa dhambi zake, akaichukia dhambi na kukusudia kuicha kabisa moyoni, akatamani na kukubali kupokea kwa njia ya imani maisha matakatifu ya Kristo. Hapo ndipo haki ya Kristo inapowekwa badala ya dhambi za mtu, na anahesabiwa kuwa mtakatifu. Yaani, ni lazima tukubali kubadilishana na Bwana Yesu - sisi tumpe dhambi zetu zote, na yeye anatupatia maisha yake matakatifu. Huku ndiko kutubu kwa kweli kutakakomfaa mdhambi. Je, mwanadamu anaweza kulifanya hili yeye mwenyewe? La. Mungu pekee ndiye anayelianzisha ndani ya mdhambi (soma Mathayo 5:30-31; 4:12, Waefeso 2:8-9). Kumbuka Mwanzo 3:15 na Waebrania 12:2-3. Ndipo tutakapoona upendo huu mkuu wa Mungu kwetu unatupatia amani na Mungu. Na ni amani hii ya Kristo moyoni inaweza kutupatia furaha ya kumtii Mungu maishani. Mtu anapokuwa amehesabiwa haki (amesamehewa dhambi) (soma Warumi 4:6-8), Mungu anafanya kitu kingine zaidi kwa mtu huyo (soma Ezekieli 36:25-27, Yohana 3:7-8, 2 Kor. 5:17, Waebrania 8:10). Mtu anazaliwa mara ya pili (upya) na anakuwa kiumbe kipya. Na mtu anapokuwa kiumbe kipya, ataishi maisha mapya, siyo yale ya zamani. Maana si yeye atendaye, bali ni Kristo atendaye kazi ndani yake kwa njia ya Roho Mtakatifu (soma Wagalatia 2:20, Yohana 15:1-5, Wafilipi 2:13, Warumi 6:17-18, 22). Kwa hiyo mtu anaendelea kukaa katika utakaso, na Mungu mwenyewe akiwa ndiye mtendaji, mwanadumu anadumu kuwa mpokeaji kwa njia ya imani, maana Mungu ndiye mwanzilishi na mkamilishaji wa imani yetu (soma Waebrania 12:2). Hadi hapo bado mwanadumu hana la kujisifia, maana matendo hayo si yake mwenyewe (soma Warumi 3:27), bali ni Roho wa Kristo aliye ndani yake (soma Wagalatia 5:22-25).

Wengi wanaweza kufikiri kuwa tayari wamempokea Yesu kwa maana halisi inayoelezwa na maandiko. Lakini unajua watu wa Mungu wa Kanisa la Mitume waliupindua Ulimwengu wa wakati ule kwa injili ya milele? Je, kile kilichofanyika wakati ule, unakiona leo? Unajua kwa nini hali ile ilikuwa tofauti na hii ya sasa? Hebu soma na kutafakari mafungu haya kwa makini. 2 Kor.5:14-15 inasema, “Maana, upendo wa Kristo watubidisha, maana tumehukumu hivi, ya kwamba mmoja alikufa kwa ajili ya wote, basi walikufa wote; tena alikufa kwa ajili ya wote; ili walio hai wasiwe hai tena kwa ajili ya nafsi zao wenyewe, bali kwa ajili yake yeye aliyekufa akafufuka kwa ajili yao”. Unakumbuka ile sheria kuu ya mbinguni? Ni Upendo usio na ubinafsi.

Kanisa la nyakati za mitume walipotambua upendo wa Mungu kwa ajili yao katika Kristo Yesu, walijitoa, Walijisalimisha kwa Mungu, wao na vyote walivyokuwa navyo (soma Warumi 12:1). Ndipo mbingu zikawamwagia roho Mtakatifu siku ya Pentekoste, ambayo matokeo yake yaliupindua ulimwengu (soma Matendo 17:6). Waumini walipokuwa wakitoa nyumba zao, wakiuza viwanja na vitu vingine wakavileta miguuni pa mitume, walikuwa wakionyesha upendo wa Yesu ndani yao ulivyokuwa ukibubujika. Waliishi si kwa ajili yao wenyewe, bali kwa ajili ya yeye aliyekufa akafufuka kwa ajili yao, yaani Yesu.

Ubinafsi ulitoka. Wakajazwa upendo wa mbinguni usio na ubinafsi. WAKAISHI KWA AJILI YA YESU. Je, unaweza kuthibitisha kuwa pale ulipoamini, ulijitoa kwa ajili ya hilo? Yaani ulijitoa kabisa uishi kwa ajili ya Yesu tu, si kwa faida yako mwenyewe? Je tumekuwa tayari kiasi gani kutoa mali zetu kwa ajili ya Yesu? Vipi kuhusu muda wetu – je, unatumika kwa ajili ya Yesu, iwe kwa kuhudhuria vipindi mbalimbali vya ibada nyumbani, kanisani au mahali pengine? Vipi kuhusu siku yake takatifu ya Sabato? Je, saa inapofika kati ya kumtukuza Bwana Yesu na nafsi yako, humsaliti Yesu ukamwacha na kusema utarudiana naye baadaye ukiisha timiza matakwa ya nafsi yako? Kuishi kwa ajili ya Yesu, ni kumruhusu daima katika mambo yote atimize kusudi lake jema ndani yako(soma Warumi 8:28). Unajua mtu anaweza kuingia kanisani, akabatizwa, akatunza Sabato pamoja na amri nyingine zote, akatoa zaka na sadaka, akahubiri injili na kufanya mambo mengine mengi, lakini, msukumo wa kufanya yote haya ukawa ni ubinafsi. Mara nyingi watu wa jinsi hii huhesabu yale waliyofanya na kujilinganisha na wengine, lakini hebu jipime na Yesu Kristo peke yake ndipo utayaona mambo kwa nuru ya mbinguni - nuru halisi. Isaya 64:6 inasema, “Kwa maana sisi sote tumekuwa kama mtu aliye mchafu, na matendo yetu yote ya haki yamekuwa kama nguo iliyotiwa unajisi, sisi sote twanyauka kama jani, na maovu yetu yatuondoa, kama upepo uondoavyo”. Yaani mwanadamu anaweza kutenda matendo yanayoonekana kuwa ni ya haki lakini bado ni mwovu tu. Dhambi imetuchafua kiasi kwamba pasipo damu ya yesu kamwe hatuwezi kuwa safi (soma Waebrania 9:22). Dhambi imo ndani yetu na haiwezi kuondolewa kwa namna yoyote tunayoweza kufanya (soma Warumi 7:7-10, 18). Sheria ya Mungu ya upendo, iletayo uzima, ndani yetu inaleta mauti. Asili ya dhambi ndiyo tuliyorithi kwa baba yetu Adamu, na katika hali hiyo kamwe hatuwezi kuwa wana wa Mungu, isipokuwa tunakubali kuingia na kuzaliwa kwa Adamu wa pili, yaani Kristo (soma Warumi 5:17, 1 Korintho 15:45-49). Hebu fikiria, kama leo ungeamua kuacha matendo yote maovu uliyokuwa unafanya na kuanza kutenda mema, je maovu yako yaliyopita ungeyaondoaje? Au ukisema matendo yako mema ya sasa yatafidia yale maovu, je ungefuta kumbukumbu lake? Soma Yeremia 2:22. Ni kwa kumpokea mwanakondoo wa Mungu tu, ndipo dhambi zetu zinaondolewa. Kufanya vinginevyo ni sawa na kukiosha kikombe kwa nje na ndani kikabakia ni kichafu. Ni pale kikombe kinapooshwa ndani, ndipo na nje huwa safi (soma Mathayo 23:25-26). Kutafuta kuhesabiwa haki kwa matendo ya sheria ni unafiki na ndio maana ni machukizo kwa Bwana. Mtume Paulo anasema, alipotambua kuwa hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki mbele za Mungu kwa matendo ya sheria, wao waliokuwa Wayahudi walimwamini Yesu (soma Wagalatia 2:15-16). Je, Paulo alipomwamini Yesu hakuwa na dini au matendo mema? Hebu soma Wafilipi 3:4-7, anasema, “Walakini mimi ningeweza kuutumaini mwili, mtu yeyote akijiona kuwa anayo sababu ya kuutumainia mwili (yaani matendo) mimi zaidi. Nalitahiriwa siku ya nane, ni mtu wa taifa la Israeli, wa kabila ya Benyamini, Mwebrainia wa Waebrainia, kwa habari ya kuishika torati, ni farisayo, kwa habari ya juhudi, mwenye kuliudhi kanisa, kwa habari ya haki ipatikanayo kwa sheria sikuwa na hatia. Lakini mambo yale yaliyokuwa faida kwangu, naliyahesabu kuwa hasara kwa ajili ya Kristo.” Paulo anatuonyesha matendo yake mema ya kidini aliyokuwa nayo, na haya ndiyo aliona si kitu, ni hasara tu. Fungu la 8 anasema, “Naam, zaidi ya hayo, nayahesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya uzuri usio na kiasi kwa kumjua Kristo Yesu, Bwana wangu, ambaye kwa ajili yake nimepata hasara ya mambo yote nikiyahesabu kuwa kama mavi ili nipate Kristo”. Mpendwa! Unaweza kuhesabu matendo yako mema yote uliyotenda nje ya Kristo (haki kwa imani), kuwa kama mavi? Tafakari kwa makini sana jambo hili, je utakuwa tayari kuachana na haki yako binafsi?

Unajua, wanadamu wote kwa asili tunajaribu kutenda mema ili, kwanza, Mungu atupatie nafasi mbinguni, tukayapate mema ya huko. Pili ni ili asije akatutupa motoni siku ya mwisho HUU NDIO UBINAFSI UNAOSEMWA. Yaani tunaamini kwa kumpokea au kumkiri Yesu kule tunakofanya ni kama kuingia shindano la bahati nasibu. Kwa hiyo Bwana Yesu ni kama tiketi ya kuingilia shindano, halafu kila mmoja sasa akazane mwenyewe kuepuka jehenamu na kupata mbingu kwa matendo yake. Ndiyo maana maneno kama “imani na matendo yako ndiyo yatakuokoa” husikika miongoni mwetu. Lakini kumbuka ndani yetu hakuna lolote jema. Na kwa sababu kujipatia haki ya Mungu kwa bidii

zetu wenyewe haiwezekani, (lakini ndicho wanadamu tunachojaribu kufanya, maisha ya kutaka kumfuata Yesu yamekuwa magumu na mzigo kwetu, mwisho ni kukata tamaa, lakini kumbuka mpendwa, "Injili ni habari njema," yaani - KATIKA KRISTO YESU, MUNGU AMETUPATANISHA NAYE, YAANI AMETUPATIA TOBA, AMETUSAMEHE KABISA DHAMBI ZETU NA KUIONDOA HATIA YETU, AMETUHESABIA HAKI NA KUTUPATIA UZIMA WA MILELE (soma Yohana 3:16-17; 2 Kor. 5:18-19). Katika Kristo Yesu mbingu zimetoa vyote na kutupatia vyote tunavyohitaji, hakuna upungufu (soma 2 Petro 1:3-4). Tusipoamini na kuupokea ukweli huu, kamwe hatutakuwa na amani ya Kristo mioyoni (soma Yohana 14:27; Mathayo 11:28-30. Tukiupokea ukweli huu ndipo tutamtumikia Mungu kwa furaha, kwani tunafurahia wokovu wetu. Na kwa vile tunapomwamini yesu, ni kuwa anaingia ndani yetu nasi ndani yake, basi matendo hayo mema hayawi yetu sisi, bali ya Kristo aliyemo ndani yetu, ndipo sifa zote na utukufu vitamrudia Mungu, naye atatukuzwa (soma Mathayo 5:16; Yohana 15:1-8)**. KUMBUKA, KUSUDI LA MAISHA LIWE KUMTUKUZA MUNGU DAIMA.**

Tofauti ya Haki Hizi:

Ili kutambua tofauti kati ya Haki kwa imani na Haki kwa matendo ya sheria, mtu hana budi kutambua asili ya jambo lenyewe. Lakini kwa maelezo machache yanayoweza kutoa mwanga kuelewa jambo lenyewe ni kuwa:

1. Haki kwa Imani - ni kitendo cha mwadanamu kukubali kupokea kwa njia ya imani kile ambacho Mungu amemfanyia katika Kristo Yesu, kwa ajili ya wokovu wake. Na hii huhusisha kuhesabiwa haki (Msamaha wa dhambi), haki ya Kristo kuwa maishani (utakaso) (au kuiishi haki ya Kristo) na mwisho kuurithi uzima wa milele (kutukuzwa pamoja na Kristo). Yaani tangu mwanzo hadi mwisho Mungu ndiye mtendaji kupitia kwa Kristo na mwanadamu ni mpokeaji tu (kuamini).

2. Haki kwa Matendo ya sheria - hapa ni kitendo cha mwandamu kutumainia kile alichotenda, anachotenda sasa na atakachotenda baadaye kulingana na sheria inavyotaka atende, ili kujiokoa. Kwa hiyo mtu mwenyewe (nafsi) ndiyo mtendaji mkuu. Ndiyo sababu ya dhana kuwa "Mungu anasaidia wanaojisaidia". Lakini kama unakumbuka kile Isaya 1:6 inachosema, utagundua kuwa kwa kweli mtu hana chochote anachoweza kujisaidia mwenyewe maana amekufa (soma Waefeso 2:5). Sasa ni maiti gani inaweza kufanya chochote? Hakika hakuna. Ndiyo maana kamwe haki hii binafsi haiwezi kumpatia mwanadamu wokovu, yaani atoke dhambini na kuitimiza haki ya Mungu. Haiwezekani kwani chochote anachofanya mtu hapo ni kwa sababu ya nafsi yake na wala si kwa ajili ya utukufu wa Mungu aliye asili ya vyote tulivyo navyo.

IMANI:

Maandiko matakatifu yanasema "Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana," (Waebrania 11:1). "Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza, kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao," (Waebrania 11:6).

Lakini imani ni nini pia. Ni mkono (Kiroho) wa mwanadamu wa kupokelea ahadi za Mungu. Yaani ni kwa njia ya imani tu mwanadamu anaweza kupokea ahadi za Mungu kwake. Hivyo isieleweke kuwa imani ndiyo mwokozi. La, bali ni njia yetu kuupokea. Na pia hiyo(imani) haitokani na sisi wenyewe, bali ni kipawa cha Mungu (soma Waefeso 2:8-9, Waebrania 12:2). Imani ni msingi wa maisha ya kumcha Mungu, maana amesema pasipo hiyo haiwezekani kumpendeza. Ndiyo maana matendo ya haki tunayoweza kutenda, pasipo imani, bado ni machukizo tu. Yatakuwa hayajatimiza ile kanuni ya mbinguni ya "Upendo usio na Ubinafsi:" Imani ni kumwamini Mungu kabisa kwa kila jambo na kumtegemea yeye tu. Tunaweza kusema kuamini ni KUJISALIMISHA KWA MUNGU. Mtu unapojisalimisha, huwa hakuna unachobakiza. Unajitoa kabisa kwa yule unayejisalimisha kwake ili akutendee apendavyo. Ni hakika tunahitaji kujisalimisha kwa Mungu ili atutendee kama apendavyo. Na tunafanya hivyo kwa kujua wazi kile anachotaka kutufanyia kwa kuwa yeye ni

mwaminifu, tofauti na ambavyo unaweza kufanya kwa mwanadamu anayebadilika-badilika. Imani kwa Mungu ni jambo la hakika (soma Waebrania 11:1), sio bahati nasibu. Kwa kweli wanadamu wengi sana tuna kitu kama bahati nasibu katika Ukristo wetu, wala hatuna hakika (imani) na Mungu. Yaani tunafanya majaribio. Tukipata, bahati nzuri, tukipoteza au kukosa, bahati mbaya. Ukitaka kuhakikisha ukweli huu, hebu jaribu kutafakari maombi yako mwenyewe na kile moyo wako ulicho na uhakika nacho. Kwa mfano, unapoomba, ukaungama dhambi zako zote, na kueleza mengine unayoyahitaji kwa Mungu, halafu unasema kwa jina la Yesu, Amina. Je moyoni mwako unaamini (una hakika) kuwa ndivyo Mungu alivyofanya au atakavyofanya? Yaani Je, unaamini kuwa Mungu amekusamehe kabisa dhambi zako na sasa anakuhesabu kuwa mwenye haki (mtakatifu) na kuwa sasa hivi au saa hiyo hiyo tayari amekupatia uzima wa milele? Je, tunafanya maombi ili Bwana atutendee mambo fulani, halafu mengine tutakamilisha wenyewe? Sasa kwa sababu hatuna hakika kuwa kwa upande wetu tutafanya bila kukosea, basi hata Mungu tuna mashaka naye kama kweli atatenda kama alivyoahidi. Ndiyo maana, kwa kweli, wengi wetu hatuna imani kwa Mungu wetu kwa kipimo cha mbinguni. Tafakari swali la Bwana Yesu "---- Walakini, atakapokuja mwana wa Adamu, je! Ataiona imani duniani," (Luka 18:8)? Bwana Yesu hakuwa anazungumzia dhana ya imani ambayo ndiyo tuliyonayo watu wengi, lakini alikuwa akisema juu ya imani ya kweli ya Mungu (Haki kwa imani); imani ya Yesu (soma Ufunuo 14:12). Hii humpatia mpokeaji imani ya kweli moyoni - amani na Mungu.

Wapendwa, Shetani anachocheza nacho maishani mwetu ni imani zetu. Maana hutuletea udhaifu wetu na dhambi zetu tulizozitenda mbele yetu na kutushawishi kuwa Mungu hawezi kabisa kumkubali mtu mwovu. Hivyo unafuata ushauri wake mwingine kuwa, bora uendelee tu na maisha hayo ya dhambi, na hivyo Mungu anadumu kuwa adui yetu. Na kama Shetani atashindwa kutufanya tusimwamini kuwa Mungu atatupokea wadhambi, ataleta fundisho jingine, nalo ni la kujitahidi kuokolewa kwa matendo ya sheria. Anasema Mungu hafanyi kila kitu, sasa kazana kwa matendo matakatifu ili Mungu akupe maksi na uwe mshindi. Sasa tahadhari ni hii, katika hili la pili anafaulu sana, maana inaonekana kana kwamba ni ukweli, naye anakuja kama malaika wa nuru (soma 2 Korintho 11:13-15). Lakini kumbuka neno la Mungu linasema, "kwa sababu hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki mbele zake kwa matendo ya sheria ----" (Warumi 3:20. Soma pia Wagalatia 2:16). Shetani akiishafaulu kuyumbisha imani yetu, matunda tutakayozaa daima yatakuwa najisi, yasiyokubalika mbele za Mungu, yamechafuliwa na ubinafsi.

Lakini jambo tunalopaswa kufahamu ni kuwa imani sio swala lililo na mpaka kwamba watu wa kundi fulani au dhehebu fulani ndio wenye imani ya kweli au imani bandia, hili ni swala la moyo wa mtu kuhusu kile anachoruhusu akipokee.

Nataka niweke neno hili wazi kwamba msingi wa mafundisho ya imani zote duniani - zile za madhehebu mengine na dini nyingine ni haki kwa matendo ya sheria. Ni msingi wa mafundisho ya neno la Mungu kama lilivyofunuliwa kwa kanisa lake la Masalio (soma Ufunuo 12:17) ndiyo unaofunua ukweli wa haki kwa imani. Lakini jambo moja la kusikitisha ni kuwa, mafundisho au ukweli huu umechafuliwa na Shetani, na sasa wengi sana tunafahamu kuwa wokovu wetu unategemea matendo yetu ya sheria. Mafundisho mengi tunayotoa yemejengwa katika mtazamo huo, na ndio maana tumekuwa watumwa wa haki hii – binafsi - ambayo tunagundua kwamba ni mzigo mkubwa, tusioweza kubeba. Kumbuka maneno ya Bwana Yesu katika Mathayo 23:4, "Wao hufunga mizigo mizito na kuwatwika watu mabegaani mwao; wasitake wenyewe kuigusa kwa kidole chao." Sasa kwa sababu ya kuwa na mafundisho hayo bandia, wengi sana wamejitenga na Mungu mioyoni. Lakini, kwa upendo, anataka kuondoa mafundisho hayo potofu, na njia pekee anayoitumia ni haki ya Kristo ambayo ni haki ya Mungu ipatikanayo kwa njia ya imani katika Kristo Yesu. Kila mmoja wetu na afanye uamuzi kuchagua ni upande gani atakayosimama.

Wako wengi ambao hawatakubali kuifukuza haki yao binafsi iliyo ya sheria ili kuipokea haki ya Kristo kwa imani; watajitenga na Kanisa la Mungu kabisa na kuwa maadui wakuu wa ile kweli ya Kristo Yesu.

Tunapohitimisha sehemu hii inayohusu imani, hebu tukumbuke na kufahamu kwamba "Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana." Kuamini ni kujisalimisha kwa Mungu kulingana na alivyojifunua katika neno lake (Upendo). Maana roho Mtakatifu huanzisha imani ndani yetu kwa njia ya neno la Mungu - Injili - (soma Warumi 10:17). Mpendwa mwombaji, hebu tutafakari kwa makini ujumbe huu tunaoendelea kujifunza. Hebu tutathmini imani zetu kwa nuru ya neno la Mungu ili isije kuwa tunapiga mbio bure (soma 1 Korintho 9:26, 2 Kor. 13:5).

IMANI NI ITIKIO LA SHUKRANI LA MOYO WA UPENDO KWA MUNGU KWA UPENDO WAKE ALIOUONYESHA KWETU PALE MSALABANI. NI KUMPENDA MUNGU KWA VYOTE BILA KUBAKIZA CHOCHOTE

KAFARA YA YESU:

Mara nyingi ni rahisi kwetu kuiangalia kafara ya Kristo kwa tukio la msalabani tu, yaani Kalvari. Lakini hebu tutafakari maneno ya Wafilipi 2:5-8, "kuweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwemo pia ndani ya Kristo Yesu; ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu; tena alipoonekana anaumbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba" Maneno haya yanatupatia sura halisi ya kile ambacho dhambi ilikisababisha kwa Uungu.

Bwana Yesu, ambaye neno la Mungu linasema ni Mungu, yaani ni mmoja wa nafsi za Uungu, alifanyika mwili, yaani alitwaa ubinadamu (soma Yohana 1:14,18). Jambo hili kwa kweli ni zaidi ya akili zetu kulipima na kulielewa jinsi lilivyofanyika. Mungu kutwaa ubinadamu, akazaliwa kama mtoto mchanga wa kibinadamu! Ajabu kwa akili zetu za kibinadamu. Soma Mathayo 1:18-23, Luka 1:26-37; 2:4-14. Kwa hiyo tunaweza kuona ukuu wa kafara ya Bwana Yesu kwa kutambua kuwa yeye ni Mungu, lakini "hakuona kule kuwa sawa na Mungu ni kitu cha kushikamana nacho" (Wafilipi 2:6b). Isije ikafikiriwa kuwa kwa kufanya hivyo Yesu aliudharau Uungu wake. La, bali inaonyesha ni kwa kiasi gani mwanadamu ni wa thamani mbele za Mungu. Na kama mwanadamu yeyote atafanya dharau kwa Bwana kwa kufikiria hivyo atakuwa anafanya kosa kubwa sana. Kwa hiyo muumbaji aliyemuumba mwanadamu, akajishusha ili kutuokoa. Kwa hiyo tangu nia ilipokuwamo ndani yake na akajitoa ili atuokoe, tayari kile kilichofanyika msalabani kilikuwa kimeanza - Yaani Mateso.

Ubinadamu wa Yesu:

Unajua, tatizo letu kuu wanadamu ni kutoamini, yaani kutomwamini Mungu. Na unajua hili ndilo lilikuwa hasa jaribu la shetani kwa Hawa, na ndio msingi wa majaribu yake yote kwetu. Sasa kwa sababu hiyo, hata kile ambacho Mungu amesema katika neno lake, ni vigumu sana kukiamini; na mojawapo ni kuhusu Ubinadamu wa Yesu. Wengi wetu tumeendelea kuamini kuwa Bwana Yesu hakutwaa mwili hasa, yaani hakuwa mwanadamu kama sisi, na kwa jinsi hiyo hata kile alichofanya katika hali yake ya ubinadamu hakina uzito sana maana inaonekana kana kwamba ni kiini macho tu.

Hebu tuone neno la Mungu linavyosema. Labda, kwa kuanzia, tuone kile Isaya anachosema (Isaya 9:6). "Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume: Na uwezo wa kifalme utakuwa begani mwake; naye ataitwa jina lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa Milele, Mfalme wa amani". Kama nilivyotangulia kusema, mtu yeyote anayefanya dharau juu ya ubinadamu wa Bwana Yesu anafanya dhambi kubwa. Unapotafakari maneno ya fungu hilo yanaonyesha wazi kuwa, ijapokuwa mtoto huyu anayezaliwa ni mwanadamu, tena mwanamume, lakini bado anaitwa, Mshauri, Mungu, Baba na Mfalme! Cheo chake cha uungu kiko palepale. Sasa, kuna watu ambao wanamchukulia Bwana Yesu kama wao wenyewe, (sisemi kama mwanadamu, bali kama wao wenyewe) yaani, kile wanachofikiri, kusema au kutenda, ndivyo wanavyomfanya Kristo awe. Lakini hili ni kosa. Ijapokuwa alitwaa ubinadamu, lakini aliishi maisha tofauti na sisi katika

kufikiri kwake, kusema kwake na kutenda kwake. Je, hii haionyeshi kuwa lazima angeishi tofauti na sisi maana yeye ni Mungu? La, yeye mwenyewe alisema “Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda ----” (Yohana 5:19). “Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe ----” (Yohana 5:30), “kwa kuwa mimi sikushuka kutoka mbinguni ili niyafanye mapenzi yangu, bali mapenzi yake aliyenipeleka” (Yohana 6:38). Ndio maana, kama mwanadamu yeyote, alihitaji msaada wa Mungu. Ndio maana alijazwa Roho Mtakatifu, na Roho ndiye akawa kiongozi wake (soma Mathayo 3:16, 4:1). Tofauti ya ubinadamu wake iliyo wazi ni kuwa - daima siku zote, Yesu alitii uongozi wa roho Mtakatifu - alifanya mapezi ya Mungu (soma Yohana 8:28-29). Hakutenda dhambi (soma Waebrania 4:15) na hakuwa na uadui na Mungu. Ndani yake asili mbili ziliunganika. Jambo la msingi kufahamu ni kuwa ili ukombozi wetu ufanyike, ilikuwa lazima Yesu kutwaa ubinadamu. Kwani, kama vile Mungu alivyoumba wanadamu wote katika au ndani ya Adamu (soma Matendo 17:26), Vivyo hivyo katika mpango wa ukombozi alituunganisha sote (ubinadamu wote) ndani ya Kristo (soma Waefeso 2:16). Kwa hiyo tendo la Bwana Yesu kufanyika mwili, ni kuunganisha wanadamu wote ndani ya uungu, na ndio “Imanueli” yaani “Mungu pamoja nasi” (Mathayo 1:23). Ni kwa kutambua na kulipokea neno moyoni, ndipo kafara ya Kristo inapoleta sura halisi katika ufahamu wetu, maana kufanyika kwake mwanadamu kumetufungamanisha naye kama ndugu yetu (soma Waebrania 2:11). Kristo hakufanya badala yetu, bali kwa ajili yetu. Ndiyo maana hakuna chochote tunachoweza kufanya nje ya Kristo kwa ajili ya wokovu wetu, maana nje yake, tunakuwa katika utu wetu wa kale ambao hauwezi kumtii Mungu (soma Waruni 7:14, 1 Kor. 2:14). Lazima Kristo awe ndani yetu nasi ndani yake kwa imani.

Muhimu: Kwa sababu haikuwezekana kabisa katika hali yetu ya dhambi kuitenda na kuitimiza haki ya Mungu, ndiyo maana kristo alitwaa mwili ili katika Yesu yote yawezekane. Warumi 8:3-4 inasema, “Maana yale yasiyowezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, Mungu , kwa kumtuma Mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi, na kwa sababu ya dhambi, aliihukumu dhambi katika mwili, ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya roho.” Kwa hiyo ubinadamu wa Yesu umefanya iwezekane kwetu wanadamu kutimiza mapenzi ya Mungu katika Kristo. Hapo nyuma tuliona kuwa kristo Yesu amefanya yote yaliyopaswa kwa ajili yetu na si badala yetu. Ndiyo maana, kumpokea au kumwamini yeye, ni kujisalimisha kwake ili atimize kusudi lake ndani yetu (soma Wafilipi 2:13). Kwa hiyo yale tunayoweza kutenda tunapoamini, hayatakuwa yetu sisi, bali ni Kristo atakayekuwa akitenda ndani yetu (soma Yohana 15:1-5). Hivyo kujisifia matendo hayo ni kutwaa utukufu wa Mungu, maana pasipo yeye sisi hatuwezi kufanya neno lolote. Kumpokea Yesu moyoni ni kufanya awe Mungu (mtawala) wa maisha badala ya nafsi kuwa Mungu.

Kuzaliwa: Malaika akasema “maana leo katika mji wa Daudi, amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye kristo Bwana” (Luka 2:11). Ni kwa ajili yetu, Kristo alitwaa mwili au ubinadamu, hivyo akazaliwa. Hivyo kuukubali ubinadamu wa Yesu ni kuonyesha imani kwake kuwa - Uungu uliungana na ubinadamu,na hivyo kupokea yote aliyofanya kwa ajili yetu. Kutoamini jambo hili ni kumkataa Kristo, na yote aliyofanya hayatakuwa na faida yoyote kwa mhusika (soma 1 Yohana 4:2.3. Hapa, katika kuzaliwa kwake ni mwanzo wa maisha yake hapa Duniani. Kupokea kwa imani mwanzo huu ni kufungua moyo kupokea huduma yake ya maisha yake yote yaliokuwa kwa ajili yetu.

Ubatizo: Kabla ya Bwana yesu kuanza kazi rasmi hapa duniani alibatizwa. Biblia inatuonyesha kuwa Yesu hakuwa na dhambi (soma 1 Petro 2:22). Lakini Yohana mbatizaji alikuwa akifanya ubatizo wa toba (soma Mathayo 3:6). Sasa kwa nini Yesu alibatizwa kama hakutenda dhambi? Jibu alilolitoa yeye mwenyewe kwa Yohana ni kuwa “kubali hivi sasa, kwa kuwa ndiyo itupasavyo kuitimiza haki yote” (Mathayo 3:15). Kwa kuliweka wazi jambo hili ni kuwa, kwa sababu Mungu aliwahesabu watu kuwa ndani ya Kristo, hivyo dhambi zetu zilikuwa ndani yake. Hivyo alifanya toba na kubatizwa kwa ajili ya dhambi zetu zilizokuwa ndani yake, yaani alizozibeba (alitubeba ndani yake) (soma 2 Kor. 5:21, Isaya 53:6). Kwa jinsi hiyo ubatizo tunaobatizwa una maana sana kuonyesha imani yetu kwa Yesu. Ndiyo maana,

kufanya kitu kingine kinyume na kile alichofanya Bwana, ni kumkataa yeye kama haki yetu na tunajipatia haki yetu wenyewe, isiyo ya Mungu. Maandiko Matakatifu yanasema hakuna wokovu katika mwingine awaye yote isipokuwa Kristo tu (soma Matendo 4:12). Na kama tumeamini, ambako ni kujisalimisha kwake ili yeye atende ndani yetu apendavyo, hakika atatuongoza kubatizwa kama yeye alivyofanya ili ile haki ikamilike ndani yetu. Kufanya kitu kinyume, kama ubatizo, tofauti na ule wa Yesu, ni sawa na sadaka aliyotoa Kaini ambayo haikuonyesha imani kwa Masihi ajaye. Ni kutoamini. Ni kwa njia ya ubatizo (kuzamishwa majini) tunapoonyesha pia kukubali mauti ya Kristo kwa ajili yetu, maana ubatizo ni kama ishara ya kuzikwa naye, na kukubali kuifia dhambi pamoja naye; na mtu hazikwi kabla hajafa. Ni wazi kuwa hii ni ishara ya kuonyesha imani yetu katika mauti yake (soma Warumi 6:2-5). Ni haki kwa imani.

Maisha Aliyoishi:

Kama mwanadamu neno la Mungu linasema hivi kumhusu Kristo "---- bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi" (Waebrania 4:15). Majaribu yote yanayotupata, Bwana Yesu aliyapitia na akayashinda. Warumi 8.3 linasema, "---- na kwa sababu ya dhambi aliihukumu dhambi katika mwili". Yaani katika mwili ulio kama wako na wangu, Kristo aliihukumu dhambi - maana yake aliishinda dhambi.

Yohana 8:29, "----kwa sababu nafanya siku zote yale yampendezayo".

Yohana 15:10, "Mkizishika amri zangu, mtakaa katika pendo langu, kama vile mimi nilivyozishika amri za Baba yangu na kukaa katika pendo lake"

Yohana 8:45, "Ni nani miongoni mwenu anishuhudiaye kuwa nina dhambi"?

Kwa hiyo, maisha Kristo Yesu aliyoishi ya mwanadamu hapa duniani yalikuwa maisha ya utii kamili kwa sheria za Mungu, ndiyo maana hakutenda dhambi. Na kwa sababu aliitii sheria kwa ukamilifu, maandiko yanasema, "Kwa maana Kristo ni mwisho wa sheria ili kila aaminiye ahesabiwa haki" (Warumi 10:4). Wengi wamelitafsiri fungu hili kumaanisha kuwa Kristo sasa ameondoa sheria na hivyo hatupaswi kuzitii au kuzitenda. Lakini Bwana Yesu mwenyewe alisema "Msidhani ya kuwa nalikuja kutangua torati au manabii, la, sikuja kutangua, bali kutimiliza" (Mathayo 5:17,19). Kwa hiyo, maana ya Kristo kuwa mwisho wa sheria ni kuwa - yeye alitii sheria takatifu ya Mungu kwa ukamilifu na hivyo sheria hiyo haimhukumu kuwa mkosaji. Sheria hiyo takatifu imeridhika kuwa matakwa yake yametimizwa. Hivyo yeyote anayemwamini Yesu, yaani anayempokea Yesu moyoni, hupewa uwezo wa kuzitii sheria za Mungu kwa ukamilifu - maana Kristo aliye ndani ya muumini huyo huzitii sheria ndani yake na hivyo anasimama mbele za Mungu kama mtu mtakatifu, yaani sheria haitamhukumu kuwa ameivunja. Kumbuka, si haki ya mtu binafsi, bali ni ya Kristo aliye ndani yake (soma Rum. 8:1).

Mauti ya Msalaba:

Katika kitabu cha Wafilipi 2:8 tunasoma, "tena alipoonekana ana umbo kama mwadanamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti naam, mauti ya msalaba".

- Waebrania 2:14 inasema, "Basi kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani Ibilisi".

- Kwa nini mauti ilikuwa lazima kwa ajili ya ukombozi wetu? Ni kwa sababu ndiyo njia ambayo kwayo Ibilisi angeharibiwa na nguvu zake. Kumbuka mwanzo 3:15 Kumponda kichwa yule nyoka wa zamani. Ufunuo 12:11 " Nao wakamshinda kwa damu ya mwanakondoo na kwa neno la ushuhuda wao ----".

- katika maisha yake hapa duniani, daima Yesu Kristo alikabiliwa na vita vile vilivyoanzia kule mbinguni. Ndani yake kulikuwa na mashindano makuu - atende kama mapenzi ya Baba yake yalivyotaka ili mwanadamu aokolewe, au atende kama nafsi yake ilivyotaka ili ajiokoe mwenyewe na mwanadamu apotee milele. Waebrania 12:2 linasema, "tukimtazama Yesu, mwenye kuanzisha na kutimiza imani yetu, ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake, aliustahimili msalaba na kuidharau aibu----."

- Pale bustani ya Gethsemani Yesu aliomba kuwa "ikiwezekana kikombe hiki kiniepuke, walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe" (Mathayo 26:39). Alipokuwa mbele ya Pilato alisema "----Mimi nimezaliwa kwa ajili ya haya, na kwa ajili ya haya mimi nalikuja ulimwenguni ili niishuhudie kweli----" (Yohana 18:37).

Mungu ashukuriwe. Kristo alistahimili msalaba, naam mauti ya msalaba. Pale msalabani Kristo aliposubiliwa, Shetani alitoa matukano makuu kupitia kwa makutano waliokuwa pale ili ikiwezekana Kristo ashuke msalabani na mwanadamu apotee milele - asiokolewe. Hebu soma jinsi ilivyokuwa (Mathayo 27:40-44), "Ewe mwenye kulivunja hekalu na kulijenga kwa siku tatu, jiokoe nafsi yako; ukiwa ndiwe mwana wa Mungu, shuka msalabani. Kadhalika na wale wakuu wa makuhani wakamdhihaki pamoja na waandishi na wazee, wakisema, aliokoa wengine, hawezi kujiokoa mwenyewe. Yeye ni mfalme wa Israeli; na ashuke sasa msalabani, nasi tutamwamini. Amemtegemea Mungu; na amwokoe sasa, kama anamtaka, kwa maana alisema, mimi ni mwana wa Mungu. Pia wale wanyang'anyi waliosulibiwa pamoja naye walimshutumu vile vile." Maneno haya makuu yakasemwa na wanadamu ambao ndio Kristo alikuja kuwaokoa!! Tusije tukawalaumu Wayahudi hawa waliofanya hayo tukifikiri sisi ni wema kuliko wao. Kama wewe au mimi tungekuwepo pale, yawezekana kabisa tungeshiriki kusema maneno hayo. Halafu pia, jambo la muhimu kutambua na kukumbuka ni kuwa Bwana Yesu alikufa, si kwa ajili ya watu fulani tu, bali ni kwa dhambi za ulimwengu wote. Dhambi zetu ndizo zilimsulibisha na kumuua (soma Isaya 53). Maneno yaliyopigiwa msitari katika fungu hapo juu yanaonyesha vita kuu ambayo kila mwanadamu amekuwa nayo na atakuwa nayo hadi mwisho.

Navyo ni vita dhidi ya nafsi. Unajua kama Yesu angeokoa nafsi yake, sisi sote tungepotea milele!! Kama Mungu angemwokoa mwanawe pale msalabani asife, wewe na mimi ndio tungekufa kifo kile. Lakini kwa Upendo mkuu usio na kifani, Mungu Baba akakaa kimya na mwana wake, Yesu, akafa (soma Mathayo 27:46), ili wewe na mimi tuokolewe na kuurithi uzima wa milele. Kwa upendo huo mkuu Kristo naye hakushuka msalabani kama shetani alivyotaka kupitia kwa wale makutano (soma Warumi 5:6-8). Pamoja na yote hayo aliyofanyiwa, sikiliza alichosema Yesu; "Baba uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo----" (Luka 23:34). Upendo ulioje!!! Mwisho, Kristo alikufa msalabani (soma Mathayo 27:50-54). Bwana Yesu hakuendelea kubaki kaburini. Siku ya tatu alifufuka (soma Mathayo 28:1-6, Marko 16:1-6, Luka 24:1-6). Je, unajua Yesu Kristo amekufa msalabani ili tusije tukafa mauti ya pili au ya milele katika jehanamu ya moto? Ni nini kitakuzuia usimpokee Yesu kuwa Bwana na mwokozi wa maisha yako? Yeye alisema "aaminiye na kubatizwa ataokoka, asiyeamini, atahukumiwa" (Marko 16:16).

Kwa nini, basi, kuna dini au imani zinazofundisha kuwa Yesu Kristo si mwokozi na pia hakufa msalabani? Jibu ni kuwa, ni kwa sababu yule adui, yaani Shetani aliamua kuwapoteza wanadamu kupitia jina la dini. Kumbuka alipomdanganya Hawa hakumwendea moja kwa moja kama Shetani, alimtumia nyoka na Hawa akadanganyika. Kama angewashawishi wanadamu kumkataa Mungu kabisa, angegundulika kwa urahisi lakini sasa yeye hujifanya malaika wa nuru ili kunasa wanadamu (soma 2 Wakorinto 11:13-15). Bwana Yesu ndiye ambaye Shetani anamchukia, lakini pia yeye Yesu ndiye mwokozi. Hivyo Shetani atampinga kwa njia yoyote ile ili mpango wa Mungu usitumie. Lakini Mungu ashukuriwe - Yesu ameshinda. Mpendwa msomaji, je, utamruhusu Kristo awe Bwana na mwokozi wako, au nafsi yako mwenyewe? Kumbuka, Mungu asipotutawala na tukafanya mapenzi yake, nafsi ndiyo itakuwa mungu kwetu na tutatenda kulingana na nafsi itakavyotuongoza. Lakini kumbuka kuwa daima nafsi ina uadui na Mungu ndiyo maana ili kumfuata Yesu, lazima nafsi isulibiwe (soma Luka 9:23-25, 14;26-27.

HUDUMA YA PATAKATIFU

Miongoni mwa huduma ya lazima kwa wokovu wa wanadamu, lakini ambayo watu wengi, sana sana hawaijui, ni hii ya Patakatifu. Yawezekana wewe u mmoja wao. Kwa hiyo, kabla hatujafika mwisho wa masomo haya, napenda kukupa fursa hii ili upate kuifahamu huduma hii muhimu.

Katika kitabu cha Kutoka 25:8 tunasoma jinsi Mungu alivyomwambia Musa, "Nao na wanifanyie Patakatifu ili nipate kukaa kati yao." Hivyo kwa kuitikia agizo hili, mahali palijengwa yaani Patakatifu au Hema ya kukutania au Hekalu (soma Kutoka 29:43-46, 40:1-11,7-38). Patakatifu palikuwa na vyumba viwili kwa ndani, nje kulikuwa na madhabahu ya Sadaka ya kuteketezwa na birika la kunawia makuhani, na ua uliovizingira vitu hivi vyote wa nguo ya kitani nzuri ya kusokotwa (soma kutoka 38:9). Patakatifu au hema hii ilikuwa na chumba cha kwanza kilichoitwa "Patakatifu" na chumba cha pili cha ndani kilichoitwa "Patakatifu pa Patakatifu". Katika chumba hiki cha kwanza cha "Patakatifu" kulikuwa na kinara cha taa, meza ya mikate ya wonyesho na madhabahu ya kufukizia uvumba. Katika chumba cha pili yaani Patakatifu pa Patakatifu kulikuwa na Sanduku la Agano na juu yake Kiti cha Rehema kikifunikwa na Makerubi. Kando ya sanduku kulikuwa na fimbo ya Haruni iliyochipuka. Ndani ya Sanduku la Agano kulikuwa na mbao mbili zilizoandikwa amri kumi za Mungu pamoja na mana. Vitu vyote hivi vilimwakilisha kristo na huduma yake ya ukombozi. Mtu alipotenda dhambi, alikwenda na mnyama pale hemani kwa ajili ya huduma ya upatanisho. Alipokuwa amefika kwa Kuhani (yaani mhudumu wa Patakatifu) pale madhabahuni (nje ya hema) mdhambi aliweka mikono kichwani pa mnyama na kuungama dhambi zake. Baada ya kuungama, yeye mwenyewe alimchinja mnyama yule na mnyama yule alitolewa pale madhabahuni na kuteketezwa kuwa kafara kwa Bwana. Kwa imani dhambi ilihama toka kwa mdhambi na kuwa juu ya mnyama aliyeuawa kwa ajili yake. Mtu huyu alirudi nyumbani akiwa huru. Lakini baadhi ya damu ya mnyama ilichukuliwa na kuhani hadi chumba cha patakatifu na kunyunyizia katika pazia lililotenga chumba cha patakatifu na kile cha Patakatifu pa Patakatifu, na kwa njia hiyo ile dhambi ilipelekwa mbele za Mungu kwa ajili ya hukumu. Yaani dhambi ile lazima ipate kutengwa kabisa na mtu aliyetubu. Pia kulikuwa na kafara maalum ya kutoa wanakondoo wawili mmoja asubuhi na mmoja jioni. Huduma hizi zilifanyika kila siku isipokuwa siku moja tu kwa mwaka. Ndani ya hema yaani katika chumba cha kwanza cha Patakatifu kulikuwa na huduma iliyofanyika kila siku, huduma iliyokuwa ya kufukiza uvumba (soma Kutoka 29:38-42; Walawi 1:1-9, 4:1-12).

Mara moja kila mwaka, ilifanyika huduma iliyohusisha chumba cha pili cha hema yaani Patakatifu pa Patakatifu. Huduma hii ilifanyika mara moja tu kwa mwaka ili kutakasa hema (Patakatifu) na watu pia. Siku hiyo iliitwa siku ya upatanisho. Huduma hii ilifanywa na kuhani mkuu tu. Katika siku hiyo kuhani alitoa ng'ombe kwa sadaka yake mwenyewe kufanya upanisho wa nafsi yake, ndipo afanye huduma ya upatanisho kwa ajili ya watu. Huduma hii ndiyo iliyoondoa dhambi zote za wana wa Israeli walizozitenda kwa mwaka mzima mbele za Bwana. Huduma hiyo ilihusisha mbuzi wawili – mmoja kwa Bwana na wa pili wa Azazeli. Ni huduma ambayo kila mtu alipaswa kushiriki kwa njia ya kujitaabisha roho yake (yaani kujihoji na kutubu dhambi yoyote aliyokuwa nayo ili apatanishwe na Mungu). Kama mtu yeyote asingefanya hivyo, basi siku hiyo hiyo angekatiliwa mbali na watu wa Mungu mara kuhani mkuu anapomaliza huduma ya siku ile (soma Walawi 16:1-34, 23:26-32, Waebrania 9:1-10). Unaweza kujiuliza swali - kwani huduma hiyo inahusianaje na wokovu wetu? Neno la Mungu linaonyesha kile kilichotokea siku ile Bwana Yesu alipokata roho pale msalabani - "Na tazama, pazia la hekalu likapasuka vipande viwili toka juu hata chini----" (Mathayo 27:51). Pazia hili ni lile lililokuwa linatenganisha vile vyumba viwili vya hekalu, yaani Patakatifu na Patakatifu pa Patakatifu, na hii ilikuwa ishara kuwa huduma yote iliyofanyika hekaluni ili kumpatanisha mdhambi ilikuwa imekoma hapa dunuani. Hakuna tena mwanadamu yeyote anayeweza kufanya huduma hiyo na ikakubalika maana atakuwa anapingana na Mungu, na mtu yeyote anayekwenda kwa kiongozi wa dini ili akaungame dhambi zake, pia atakuwa anapingana na Mungu na huduma hiyo inakuwa ya bure tu (soma Mathayo 15:8-9). Sasa kama huduma ile ilikoma, je mdhambi afanyeje sasa? Endelea kujifunza.

Biblia inasema, "---tunaye Kuhani Mkuu wa namna hii, aliyeketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha ukuu mbinguni, mhudumu wa patakatifu, na wa ile hema ya kweli, ambayo Bwana aliiweka wala si mwanadamu. "-----watumikao mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni, kama Musa alivyoagizwa na Mungu, alipokuwa tayari kuifanya ile hema; maana asema, Angalia ukavifanye vitu vyote kwa mfano ule ulioonyeshwa katika mlima" (Waebrania 8:1-5). "Basi ilikuwa sharti nakala za mambo yaliyo mbinguni zisafishwe kwa hizo, lakini mambo ya mbinguni yenyewe yasafishwe kwa dhabihu zilizo bora kuliko hizo" (Waebrania 9:23).

Ni wazi kuwa Patakatifu pa duniani na huduma zake ilikuwa ni nakala au mfano wa Patakatifu na huduma za mbinguni. Sasa elewa nakala hizi kwa ukaribu au uwazi zaidi:

- Mnyama kwa sadaka ya kuteketezwa ya dhambi ilimwakilisha kristo kama kafara kwa dhambi zetu (soma Yohana 1:29, Waebrania 9:13-14)

- Kuhani (mhudumu wa Patakatifu) alimwakilisha Yesu kama Kuhani wetu mkuu (soma Waebrania 8:1-2, 4:14-15).

- Kinara cha taa kilimwakilisha Yesu kama nuru halisi (soma Yohana 1:9-14, 3:19, 9:5).

- Mikate ya wonyesho iliwakilisha jinsi mwanadamu anavyopata chakula chake kwa Mungu (cha kimwili na cha Kiroho) kwanjia ya Kristo (soma Yohana 6:31-33).

- Madhabahu ya kufukizia uvumba iliwakilisha huduma ya Yesu ya kutuombea (soma Waebrania 7:25, 1Yohana 2:1).

- Sanduku la agano (Amri Kumi) iliwakilisha tabia takatifu ya Mungu na kanuni pekee ambazo wanadamu wanapaswa kuzitii. Utakatifu huo ndiyo "haki ya Kristo" (soma Kutoka 19:5-6, Ezekieli 20:11-12).

- Kiti cha Rehema ni mahali ambapo utukufu wa Mungu (Shekina) ulionekana juu ya lile Sanduku la Agano. Hii inaonyesha kuwa enzi yake Mungu wetu imejengwa katika sheria zake ambazo ndio tabia yake (soma Lawi. 11:44, Zaburi 45:6-7). Ni mfano wa kiti cha enzi cha mbinguni.

- Mbuzi wa Sadaka ya dhambi kwa ajili ya bwana (siku ya upatanisho) alimwakilisha Kristo kama kafara ya Bwana kwa dhambi.

  Mbuziwa Azazeli (siku ya upatinisho) alimwakilisha Shetani.kuhani Ni kwa mkuu alipokuwa amekwishamtoa ng'ombe wa sadaka ya dhambi kwa ajili ya nafsi yake na kufanya huduma zilizofuata, alikuwa akitoa pia mbuzi aliyekuwa sadaka ya dhambi kwa ajili ya upatanisho wa Patakatifu, kwa sababu ya makosa ya Walsraeli, na mambo yao machafu, na kwa ajili ya hema ya kukutania. Na baada ya huduma hii ambayo ilihusisha kunyunyiza baadhi ya damu ya yule ngombe na mbuzi; juu ya kiti cha rehema machafu yote ya wana wa Israeli yaliitoka madhabahu na Patakatifu (hema) (soma Walawi 16:14-19). Baada ya huduma hiyo, alifanya huduma nyingine kwa mbuzi wa pili (wa Azazeli), ambayo ilikuwa ni kuweka mikono yake juu ya mbuzi huyo na kuungama uovu wote, makosa yote na dhambi zote za Israeli (zilizotoka Patakatifu) juu ya mbuzi huyu, kisha alichukuliwa mbali jangwani na kuachwa huko. Hivyo dhambi zote zilikuwa sasa zimetengwa mbali na mkutano wa watu na Mungu (soma Walawi 16:20-28).

- Mnyama katika madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa iliwakilisha kafara ya Kristo msalabani.

- Huduma ya kila siku iliyohusisha pia chumba cha kwanza cha Patakatifu ikiwakilisha sehemu ya kwanza ya huduma ya Yesu katika Patakatifu pa mbinguni (soma Waebrania 7:26-28, 9:11-22).

  Huduma ya siku ya upatanisho (siku ya Hukumu – soma Dan.7:9-10) iliwakilisha huduma ya mwisho ya Yesu katika chumba cha Patakatifu pa Patakatifu mbinguni. Huduma hii ndiyo inayoendelea sasa. Wote wanaomwamini Yesu na kutubu dhambi zao watasamehewa na dhambi zao Yesu amezibeba, lakini atakapomaliza huduma hiyo, dhambi zote zilizoungamwa zitawekwa juu ya Shetani (mbuzi wa Azazeli) aliye mwanzilishi wa dhambi na ndiye atabeba hukumu ya dhambi hizo katika jehanamu.

  Wale watakaokataa kumpa Yesu dhambi zao (kutubu) watapaswa kubeba hukumu au mzigo wao wenyewe (soma Waebrania 9:23-28). Je, utachagua kundi gani?

Kwa hiyo sasa hivi hatuna haja ya kutoa wanyama kuwa kafara kwa dhambi maana Kristo tayari amejitoa kwa ajili yetu. Hatuna haja kwenda kwa mtu yeyote ili kuungama mbele zake, bali tunakwenda moja kwa moja kwa kuhani wetu wa mbinguni - Bwana Yesu - ili tuungame kwake. Hakuna mwakilishi. Wakati wa Patakatifu pa duniani, mdhambi alikwenda yeye binafsi kwa kuhani. Hakupitia kwa mtu mwingine ili amwombee, na hii ilikuwa nakala ya mambo ya mbinguni. Kwa hiyo tumwendee Yesu moja kwa moja kwa njia ya maombi na kuungama dhambi zetu kwake, ili yeye atuombee kwa Baba.
Jambo jingine muhimu ni kuwa ijapokuwa mdhambi aliondolewa dhambi alipopeleka mnyama wa kafara, lakini ilimpasa kushirikiana na kuhani mkuu kwa huduma ya siku ya upatanisho na utakaso kwa njia ya kujitaabisha roho yake, asije akakataliwa mbali na watu wa Mungu. Sasa wengi wanaodai kumwamini Yesu kama mwokozi, wameishia tu pale katika huduma ya kafara katika madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa (msalabani) na hawajui kuwa baada ya kutoa kafara, Kuhani wetu mkuu - Yesu - ameingia Patakatifu pa mbinguni ili kukamilisha huduma yake ya Upatanisho - ambayo ni kukomesha dhambi kabisa moyoni mwa muumini. Na kwa sababu hiyo, anasubiri kila mtu atambue ukweli huu na kufanya uamuzi - halafu atatupa chini chetezo na kumaliza kazi ya upatanisho na kupatakasa Patakatifu (soma Ufunuo 15:5-8). Mara tu Kristo atakapomaliza huduma yake katika Patakatifu pa Patakatifu pa mbinguni, atakuja mara ya pili kwa wale wamtazamiao kwa wokovu (soma Waebrania 9:28). Kwa hiyo, sasa hivi tuko katika siku kuu ya upatanisho. Kristo yuko mbinguni mbele za Baba kwa ajili yetu. Huu ni wakati wetu kujitaabisha roho zetu kwa kufanya toba kamili kwa Mungu wetu na kuwa na imani katika Kristo Yesu ili dhambi zetu zisamehewe na kufutwa na Kristo awezekurudi na kutuchukua mbinguni. Kumbuka, mioyo yetu ni hekalu ambalo Mungu anataka akae na kutawala. Je, tutamruhusu aingie na kutawala (soma Ufunuo 3:20-21)?

DHAMBI:

Katika masomo haya ambayo umeendelea kujifunza, naamini umeona wazi kuwa kilichosababisha mpango huu wa wokovu ni dhambi. Nafasi hii tena ni ya kuiangalia dhambi kwa uwazi zaidi.

- Je, Dhambi ni nini? Neno la Mungu (Biblia) linasema "Kila atendaye dhambi afanya uasi, kwa kuwa dhambi ni uasi" (1 Yohana 3:4).

- Uasi huu ni wa nini? Uasi huu ni wa torati au sheria ya Mungu (soma Warumi 7:7-8).

- Je, torati ina asili gani? "Ni takatifu, na ya haki na njema" na pia asili yake ni ya rohoni (soma Warumi 7:12-14).

Unaposoma Warumi 7:15-24, neno la Mungu limeonyesha wazi hali yetu ya dhambi. Imeelezwa kuwa imo ndani yetu na ndiyo sheria inayotawala viungo vyetu kiasi kwamba hata tukitaka kutenda lililo jema, hatupati, maana hamna jema lolote ndani yetu isipokuwa dhambi tu. Hii ni sawa na kusema nia ya miili yetu daima ni kutenda dhambi.

- Je maandiko yanasema nini kuhusu hii nia ya miili yetu? Warumi 8:6-7 inasema, "Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti, bali nia ya roho ni uzima na amani. Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu. Wala haiwezi kuitii".

Hali hii ya uadui juu ya Mungu ndiyo kila mwanadamu aliyo nayo. Ndiyo asili tunayorithi toka kwa Adamu (soma Warumi 5:12, 3:10-18, Zaburi 14:2-3). Kumbuka lilitokea pale Edeni bustanini mara Adamu na Hawa walipoasi walijikuta wamekuwa maadui wa Mungu na marafiki wa Shetani (soma Yohana 8:44, 1 Yohana 3:8). Hivyo hakuna mtu yeyote anayeweza kukanusha kuwa kwa asili yake hana uadui na Mungu. Si swala la uchaguzi ni la kurithi (soma 1 Petro 1:18). Kumbuka daima kuwa, dhambi ni ile nia ya mwili ambayo ni uasi wa sheria za Mungu, ni uadui juu ya Mungu. Ndiyo maana tunapaswa kutafakari upya juu ya maisha yetu na yote tuyawazayo, tusemayo na kuyatenda. Je, ni nia ya miili (Nafsi) yetu au ni mapenzi ya Mungu. Na ili kujua kama ni mapenzi ya Mungu au la, njia ni kuyapima kwa nuru ya neno la Mungu. Ikiwa ni sawa sawa na neno hilo, basi jambo hilo si dhambi (soma Isaya 8:20).

Siku hizi yapo mambo mengi sana yanayofanyika kinyume kabisa na neno la Mungu, na tena mengine kwa jina la dini, na watu wengi wanafikiri ni sawa tu. Wengine hujaribu kupima na kusema dhambi hii ni ndogo tu na haiwezi kumzuia mtu kuingia mbinguni. Yote haya ni hila za Shetani kuwadanganya wanadamu ili hatimaye wapotee. Usidanganyike mpendwa, Biblia inasema ,"Mungu hadhihakiwi, kwa kuwa chochote apandacho mtu, ndicho atakachovuna, maana yeye apandaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu,; bali yeye apandaye kwa Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele" (Wagalatia 6:7-8). Dhambi ndogo au moja ni nia ya mwili ambayo ni uadui juu ya Mungu. Dhambi kiasi au nyingi ni nia ya mwili ambayo ni uadui juu ya Mungu. Hivyo wote ni maadui wa Mungu na ndiyo maana hukumu yao ni moja tu - ziwa la moto. Yakobo 2:10.12 inasema, "Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote. Maana yeye aliyesema usizini, pia alisema usiue. Basi ijapokuwa hukuzini, lakini umeua, umekuwa mvunja sheria ----." Jipime katika sheria takatifu (amri kumi) za Mungu ili ujue uko kwa Mungu au kwa shetani aliye mwenye dhambi.

Kristo Yesu pekee ndiye tumaini letu la wokovu. Hebu tufungue mioyo yetu ili aingie na kutushindia dhambi. Kumbuka torati au sheria ya Mungu asili yake ni ya rohoni.

Hivyo uasi wa sheria hii pia unaanzia moyoni (soma Isaya 14:13-14, Ezekieli 28:17). Uasi ulianzia moyoni mwa Lusifa na akawa Shetani. Adamu na Hawa walitenda dhambi (kula tunda) wakati walipopoteza uhusiano na Mungu mioyoni mwao. Hivyo kula tunda ilikuwa ishara ya nje ya uasi moyoni. Badala ya kumwamini Mungu, walimwamini Shetani. Ndivyo ilivyo leo, wale wote wanaomwamini Yesu, wanapewa uwezo kufanyika wana wa Mungu. Hili si swala la kinywani tu, bali ni la moyoni pia (soma Warumi 10:9-10). Wale wanaomwasi Mungu na kumwamini Shetani wanaendelea kutenda dhambi na mwisho ni kuangamia milele (soma Ufunuo 21:8).

KRISTO AKIPOKELEWA MOYONI:

1. Atakupatanisha na Mungu kwa kuondoa ile nia ya mwili ambayo ni uadui juu ya Mungu. Nia ya mwili ndiyo dhambi (soma Waefeso 2:13-17, 1 yohana 2:2, 3:8, 1Timotheo 2:5). TOBA!

2. Utasamehewa dhambi (soma Warumi 3:25-26, Mathayo 2:37-38, 3:19, 1 Yohana 1:8-9).

3. Anakupa uwezo kufanyika mwana wa Mungu, yaani uwezo wa kutii sheria za Mungu kikamilifu (soma Yohana 1:12-13, 14:15, 15:1-8).

4. Anakupatia uzima wa milele (soma Yohana 3:16, 5:24-29, 6:39,48-58).

5. Anakupatia ushindi juu ya dhambi (soma 1 Kor. 15:57, Warumi 7:25, 1 yohana 5:3-5, Ufunuo 12:11).

Yote haya Mungu wetu ametupatia kutokana na upendo ulio mkuu kwetu wanadamu. Neno lake linasema, "mmeokolewa kwa neema" (Waefeso 2:8-9). Neema hii imefunuliwa katika Kristo Yesu. Na yeyote anayempokea Yesu kuwa Bwana na mwokozi wa maisha yake anakuwa ni adui wa Shetani maana ndani yake kuna adui ya Shetani, na vita vile vilivyoanza mbinguni vinajitokeza kwa sura ya juu zaidi. Lakini Bwana asifiwe, Kristo Yesu ameshinda.

WITO WA MWISHO WA WOKOVU KWA ULIMWENGU

Katika kitabu cha Warumi 13:12 tunasoma, "Usiku umeendelea sana, mchana umekaribia -----."

1 Petro 4:7 inasema, "lakini mwisho wa mambo yote umekaribia, basi iweni na akili, mkeshe katika sala". Mwisho wa mambo yote! Mwisho wa biashara, elimu, kazi, vyeo, kilimo, anasa, mwisho wa dunia na vyote vilivyomo. Lakini mbona mwisho huu haujafika?

2 Petro3:9 inasema, "Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake---- bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu yeyote apotee bali wote wafikilie toba."

Kwa hiyo mpendwa, Mungu wetu anayetupenda upeo. Hapendi tupotee, ndio maana ameendelea kutusubiri ili tuujue ukweli halisi, yaani ile injili ya milele au habari njema ya ufalme, halafu tufanye uchaguzi, ama kuamini au kutoamini, ndipo ule mwisho uje. Hivyo kabla ya ule mwisho, Mungu ametuletea ujumbe wa mwisho wa onyo. Ujumbe huo ndio sehemu ya mwisho ya kijitabu hiki.

Ujumbe huu wa mwisho unajulikana kama Ujumbe wa Malaika Watatu. Hebu jifunza ujumbe huu kwa makini maana ni ujumbe kwa watu wote waishio duniani.

Malaika wa Kwanza

Ufunuo 14:6-7, "kisha nikaona malaika mwingine akiruka katikati ya mbingu, mwenye injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi, na kila taifa na kabila na lugha na jamaa, akasema kwa sauti kuu, mcheni Mungu na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja, msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemichemi za maji".

- Malaika ni nani? Ni watumishi wa Mungu (soma Waebrania 1:7, Ufunuo 19:10). Hivyo malaika hawa huwakilisha watumishi wa Mungu (wanadamu) wanaotangaza ujumbe huo. Sasa hebu tutafakari ujumbe au wito wa Mungu kwa njia ya malaika huyu wa kwanza. Malaika anasema:

- "Mcheni Mungu." - Kumcha ni kumpa mhusika heshima iliyo ya juu sana. Hivyo Mungu anatuita tumpe yeye heshima iliyo kuu sana na kumpa <u>nafasi ya</u> <u>kwanza</u> katika maisha yetu badala ya kutanguliza <u>nafsi</u> ambazo hutufanya tuwe na Miungu mingine (soma Kutoka 20:3). Tutii amri zake.

- "Na Kumtukuza." - Tumpe Mungu utukufu wake. Njia ambayo kwayo tutampa utukufu ni kwa kuishi maisha matakatifu ya <u>utii</u> kamili kwa amri za Mungu. Ni kuacha dhambi na kuishi maisha ya ushindi katika Kristo Yesu (soma Mathayo 5:16, Waefeso 5:8-10, Yohana 15:8). Haki kwa imani.

- "Kwa maana saa ya hukumu yake imekuja." - Saa ya hukumu ni ule wakati au kipindi cha huduma ya Yesu katika chumba cha Patakatifu pa Patakatifu mbinguni; huduma ambayo iliwakilishwa na huduma ya siku ya upatanisho katika nyakati za huduma ya Patakatifu pa duniani kama tulivyojifunza katika somo lililohusu Patakatifu. Hukumu ni kuamua kuwa mtu huyu hana hatia hivyo yuko huru au kuwa ana hatia hivyo aadhibiwe. Kama tulivyoona, sasa tunaishi katika saa hiyo ya hukumu, katika siku kuu ya upatanisho (soma Danieli 8:14, 7:9,10,13, 1 Petro 4:17). Wale wanaomuamini Yesu wanahesabiwa haki na kukubaliwa kwa ufalme wa Mungu - Majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima. Wale wasioamini wanaandikwa katika kitabu cha hukumu (soma Ufunuo 3:5, 20:12). Saa hiyo ni sasa.

- "Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemichemi za maji." Hapa neno la Mungu linatukumbusha kuhusu ibada (msujudieni) na pia linatueleza ni kwa nini tumsujudie, linasema kwa kuwa ni Muumbaji. Unajua jambo pekee linalomtofautisha Mungu wa kweli na miungu mingine ya uongo ni uwezo wake wa uumbaji. Katika ibada ya dini nyingi duniani, watu wamekuwa wakiabudu vitu vingine badala ya Mungu wa kweli, huku wakidhani wanamwabudu Mungu Muumbaji. Je, unawezaje kujua kama unamwabudu Mungu wa kweli aliyeumba mbingu na nchi na bahari na vyote vilivyomo? Je, kuna ishara yoyote inayotajwa katika Biblia kuonyesha jambo hilo? Ndiyo, hebu tusome. Kutoka 31.13, "Hakika mtazishika Sabato zangu, kwa kuwa ni ishara kati ya mimi na ninyi katika vizazi vyenu vyote; ili mpate kujua ya kuwa mimi ndimi Bwana niwatakasaye ninyi." Ezekieli 20:12, "Tena naliwapa Sabato zangu, ziwe ishara kati ya mimi na wao, wapate kujua ya kuwa mimi, Bwana, ndiye niwatakasaye." Ezekieli 20:20, "Zitakaseni Sabato zangu, nazo zitakuwa ishara kati ya mimi na ninyi, mpate kujua ya kuwa mimi ndimi Bwana, Mungu wenu."

  Ishara hii inatuelekeza moja kwa moja katika amri ya nne kati ya zile amri kumi za Mungu. Hii ni amri ambayo watu wengi sana duniani hawaishiki, tena watu wa dini zote, wakati hiyo ndiyo ishara pekee ya kumwabudu Mungu wa kweli. Hii inaonyesha jinsi watu wengi wamekuwa wanaabudu miungu mingine badala ya Muumbaji. Lakini je amri hiyo ya nne inasemaje? Kutoka 20:8-11 inasema, "Ikumbuke siku ya sabato uitakase, siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote, lakini siku ya Saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yoyote, wewe, wala mwana wako, wala binti yao. Wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga. Wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita Bwana alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba, kwa hiyo Bwana akaibarikia siku ya Sabato, akaitakasa." Soma pia Mwanzo 2:1-3.

- Neno la Mungu halituambii kuwa tuchague siku yoyote katika wiki ili iwe Sabato. Linasema si yetu, ni ya Bwana. Siku aliyostarehe akaibariki na kuitakasa. Siku nyingine sita hazina utakaso wala mibaraka ya Sabato, hivyo haziwezi kuwa siku ya Sabato. Siku ya saba ya juma (wiki) ndiyo Sababo, na siku hiyo ni Jumamosi. Kumbuka msomaji, jambo lolote lililo kinyume na neno la Mungu ni nia ya mwili (nafsi), ambayo ni uadui juu ya Mungu, ambao ndio dhambi. Angalia ibada yako isiwe ya bure (somo Mathayo 15:8-9). Hivyo wote wanaotaka Mungu muumbaji awe Mungu wao wanapaswa kuonyesha ibada yao ya kweli kwa kuitunza Sabato na wala si vinginevyo. Wote watakaokataa ishara hii ya Sabato watakuwa wanasujudia kitu kingine. Sabato inamtofautisha na kumtangaza Mungu kama muumbaji.

- Lakini malaika huyu, pia ana injili ya milele. Injili ya milele ndizo habari njema za wokovu katika Kristo Yesu ambazo umekuwa ukizisoma katika maelezo yaliyopita. "Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo" isipokuwa la Yesu (Matendo 4:12).

- Huu ndio ujumbe ambao unatakiwa uhubiriwe kwa watu wa mataifa yote kuwa Yesu ni mwokozi pekee wa ulimwengu na wale wanaomwamini wataonyesha imani yao kwa kuzishika amri zake ikiwemo na Sabato ya siku ya saba ya juma, yaani Jumamosi.

Malaika wa Pili

Ufunuo 14:8, "Kisha mwingine, malaika wa pili, akafuata, akisema, umeanguka, umeanguka Babeli, mji ule ulio mkubwa, maana ndio uliowanywesha mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake."

- "Umeanguka." - Neno hili limetumika kuonyesha hali ya kuuacha ukweli wa neno la Mungu kama msingi pekee wa imani na kugeukia mafundisho mengine yasiyo na msingi katika maandiko (soma Mathayo 7:24-27). Hili ni anguko la Kiroho. Anguko hili limeelezwa katika ujumbe huu wa malaika wa pili kama matokeo halisi na yasiyoepukika kwa mtu yeyote au dini yoyote isiyokubali kuupokea ujumbe wa malaika wa kwanza. Kumbuka malaika wa kwanza anahubiri injili ya milele (yaani wokovu katika Kristo Yesu pekee). Anatuita tumtukuze Mungu kwa kuzishika amri zake. Anatuita tumpe Mungu heshima ya juu sana na nafasi ya kwanza katika maisha yetu, kumsujudia (kumwabudu) na kuonyesha ibada hiyo ya kweli kwa kuitunza na kuitakasa Sabato ya siku ya saba ya juma kumtukuza Mungu kama muumbaji wa mbingu na nchi na bahari na vyote vilivyomo. Huu ndio mpango wa Mungu.

  Kwa hiyo kuukataa (kutokuupokea) ujumbe huo wa malaika wa kwanza, ni kuukataa mpango halisi wa Mungu na kuanguka kiroho. Na popote neno la Mungu linapokataliwa, Shetani huingiza mafundisho ya uongo ili kuchukua nafasi hiyo. Ndiyo maana mafundisho ya dini zote tulizo nazo leo, yako kinyume kabisa na Mungu. Na ndio sababu ya kuwa na dini mbalimbali na madhehebu mengi sana tofauti, huku tukidai tunamwamini na kumwabudu Mungu mmoja. Huu ni uongo wa shetani ili kuwapoteza wanadamu (soma Mathayo 15:8-9, 2 Kor. 11:13-15). Usalama wetu ni kukubali wito wa Mungu kwetu kama unavyoelezwa katika ujumbe wa malaika wa kwanza.

- "Babeli, mji ule ulio Mkubwa." - Kwa mara ya kwanza katika Biblia mji ulioitwa Babeli ulijengwa na mtu aliyeitwa Nimrodi, ambaye alifanya vita kubwa sana dhidi ya Mungu kwa kuwafundisha watu kwenda kinyume na neno la Mungu. Alianzisha ufalme wa kwanza kabisa duniani uliokuwa kinyume na Mungu (soma Mwanzo 10:8-14). Miji hii mikubwa aliyoijenga ndiko kulikuwa chimbuko la ibada nyingi za uongo tunazoziona leo. Hebu angalia jinsi Nimrodi alivyopingana na Mungu. Katika kitabu cha Mwanzo 1:28 tunasoma, "Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi ----." Na katika mwanzo 9:11 tunasoma, "na agano langu nitalithibitisha nanyi, wala kila chenye mwili hakitafutwa tena kwa maji ya gharika, wala hakutakuwa tena gharika, baada ya hayo kuiharibu nchi." Huo ndio ulikuwa mpango wa Mungu. Lakini chini ya Nimrodi watu walifanya mpango ulio kinyume, "Wakasema, haya, na tujijengee mji, na mnara, na kilele chake kifike mbunguni; tujifanyie jina, ili tusipate kutawanyika usoni pa nchi yote" (Mwanzo 11:14). Kwa hiyo wao hawakutaka kutawanyika usono pa nchi, na pia hawakumwamini Mungu kuwa hataleta tena gharika, hivyo wakaamua kujenga mnara na kilele kifike mbinguni, ili gharika ikija tena, wapande juu ya mnara na kujiponya. Jambo jingine muhimu kulitambua ni ile kanuni iliyowasukuma kufanya hivyo. Nafsi, nafsi, nafsi, ndiyo waliyoitii, badala ya kumtii Mungu, maana walisema tujijengee, tujifanyie jina, tusipate…, - binafsi. Hii ndiyo iliyokuwa kanuni iliyomwongoza Shetani kuasi (soma Isaya 14:13-14). "Nita" "mimi"; ndiyo msingi wa anguko la mwanadamu katika dhambi, na ndio msingi wa imani au dini zote zisizojengwa katika neno la Mungu. Hiyo, ndiyo kanuni ya Babeli. Sasa, mji ule uliojengwa na Nimrodi uliharibiwa lakini mji huo wa Babeli ukajengwa tena na mfalme aliyeitwa Nabukadreza kwa kanuni ile ile ya kujitukuza nafsi kuliko Mungu (soma Danieli 4:29-32). Mji huu ulikuwa mkubwa. Ukaitwa "mji wa dhahabu," "utukufu wa dunia nzima" na ufalme huo wa Babeli ulitukuka sana. Lakini kwa sababu ya kumwasi Mungu na kutompa utukufu, mji huu nao uliharibiwa (soma Isaya 21:9, Yeramia 51:52-64). Hivyo mji huu ya Babeli unawakilisha mifumo yote ya dini za uongo zilizomwasi Mungu. Na kama mji huu halisi ulivyoanguka na kuangamia na hata leo haupo, inasimama kuwa ishara kwamba imani au dini zote zisizojengwa katika Biblia mwisho wake ni kuanguka na kuangamia milele (soma Ufunuo 18:5-24).

Ndugu msomaji, umesimama upande gani? Katika imani inayowakilishwa na Babeli, ambazo ni imani zilizoanguka; au upande wa Bwana? Hii ni nafasi yako ya pekee sana kuchagua wokovu kama unavyofunuliwa na neno la Mungu.

- "Maana --- uliwanywesha mataifa yote mvinyo--- ya uasherati wake."
- Kunywesha ni kufundisha (soma Yohana 4:14, 7:37-38).
- Mvinyo ni mfano wa mafundisho ya uongo. Kama tunavyofahamu kuwa mvinyo ni pombe au kileo, na mtu anapokunywa analewa na matokeo ya kulewa tunayafahamu. Hivyo mfumo huu wa imani au dini au mafundisho ya uongo, ambayo yana chimbuko lake katika mji wa Babeli, yameenea kwa mataifa yote na kusababisha watu kulewa na mafundisho hayo hata wasitambue kweli ya neno la Mungu. Yeremia 51:7 inasema, "Babeli umekuwa kikombe cha dhahabu mkononi mwa Bwana. Kilicholevya dunia yote; mataifa wamekunywa mvinyo wake; kwa sababu hiyo mataifa wameingiwa wazimu." Mambo ya kutisha ajabu. Kama mataifa wamekuwa na wazimu kwa sababu ya mafundisho hayo ya uongo ya kidini, je, tunaweza kushangaa ni kwa nini dunia yetu imejaa magomvi, mauaji, zinaa, ubakaji, vita, dhuluma na kuharibika kwa maadili mengine mengi? Na katika hali hiyo ukweli wa neno la Mungu unaposemwa wazi, watu hawa walio na wazimu watawatesa na kuwaua watu wa Mungu.

- Uasherati wake - huwakilisha uhusiano usio halali nje ya ndoa. Neno la Mungu huelezea uhusiano kati yake na watu wake kwa mfano wa uhusiano wa ndoa - Mungu kama mume na watu wake kama mke wake. Mambo haya ni ya kiroho na tunatakiwa kuyatambua kwa jinsi ya rohoni (soma 1Kor. 2:13-15). Uhusiano huo umeelezwa katika Yeremia 3:14, Isaya 54:5-6 na Waefeso 5:25-32. Kwa hiyo tunapomwacha Mungu wetu kwa kutolishika neno lake, ijapokuwa tuwe na dini na kuabudu, lakini tutakuwa tunaabudu Mungu mwingine asiye wa kweli, na hivyo tutakuwa tunafanya uzinzi kiroho. Kwa hiyo Babeli ilimwasi Mungu na kufundisha uongo ambao leo umeenea katika mataifa yote. Mafundisho mengi yaliyomo katika baadhi ya madhehebu ya kikristo, Uislamu, Buddha, Hindu, dini za kimila nk. ni ya uongo, na hivyo yanawakilisha Babeli (mke aliyemwasi mumewe) kiroho.

- Sasa, kama miji ile ya Babeli iliishaanguka, je, leo bado tunaweza kusema kuna mji wa Babeli? Ndiyo. Leo pia bado kuna Babeli ya sasa ambayo siyo mji bali ni mamlaka ya dini ambayo ndani yake yamejaa mafundisho ya kipagani, na mafundisho hayo yameenea katika dini mbali-mbali duniani. Hivyo badala ya mamlaka hiyo ya kidini kuwa mke wa kristo, sasa inaitwa, "Babeli Mkuu, mama wa makahaba na machukizo ya nchi" (soma Ufunuo 17:1-6). Lakini jina hili ni la siri, unaweza tu kulitambua kutokana na nuru ya neno la Mungu. Na hiyo ndiyo mamlaka ya kanisa la Rumi (Roman Catholic) kama mama, na makanisa mengine yote yanayofuata mafundisho yake kama watoto wake ambao pia ni makahaba (soma Ufunuo 17:18).

Baadhi ya Mafundisho ya Babeli ni:

1. Imani kwamba mtu ana roho ambayo haifi - huishim milele.
2. Waovu kuungua milele na milele katika jehenamu ya moto.
3. kuabudu jua, mwezi na nyota.
4. Ibada ya siku ya kwanza ya juma, yaani Jumapili.
5. Kuombea na kuomba wafu.
6. Kusujudia na kuabudu sanamu nk.

Ujumbe wa Malaika wa Tatu

Ufunuo 14:9-12, "Na mwingine, malaika wa tatu, akafuata, akisema kwa sauti kuu, mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake, naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za mwanakondoo. Na moshi wa maumivu yao hupanda juu hata milele na milele, wala hawana raha mchana wala usiku, hao wamsujuduo huyo mnyama na sanamu yake, na kila aipokeaye chapa ya jina lake. Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu na imani ya Yesu".

Malaika huyu wa tatu anauonya ulimwengu juu ya kumsujudia mnyama na sanamu yake na kuipokea chapa yake. Hukumu ya kutisha inatangazwa dhidi ya wote watakaomsujudia mnyama huyu - kutupwa katika ziwa la moto - ni hukumu ya kutisha. Kwa nini usijiepushe na mnyama huyu? Je, unamfahamu? Hebu tunapoelekea mwishoni, jifunze kumfahamu mnyama huyu.

- "Mnyama" – Biblia inatafsiri mnyama kuwa ni mfalme au ufalme (soma Danieli 7:15-17, 23-25.) Katika Ufunuo 13:11-18 inaelezea kuhusu mnyama (ufalme) utakaoilazimisha dunia na wote wakaao ndani yake wamsujudie mnyama anayeitwa wa kwanza na sanamu yake. Mnyama huyu wa kwanza ni yule anayetajwa katika Ufunuo 13:1-8. Huyu ni yule aliyepokea au kurithi mamlaka ya dola ya Kirumi (soma Ufunuo 13:1-2.) Joka ni tafsiri ya mamlaka aliyotumia Shetani ili kumwangamiza Bwana Yesu (soma Ufunuo 12:1-5) na maandiko yanaonyesha wazi kuwa mfalme wa Kirumi (Herode) alianzisha mauaji makuu ya watoto ili ikiwezekana amwangamize Yesu, lakini Mungu alimwokoa na mauaji hayo (soma Mathayo 2:13-23.) Mnyama huyu, ambaye watu wote watalazimishwa kumsujudu na ambaye ni mrithi wa kiti ch enzi cha dola ya Kirumi, si mwingine isipokuwa ni MAMLAKA YA KANISA LA RUMI au UPAPA. Hivyo neno la Mungu linafunua jambo muhimu sana kwa kila mtu aishiye duniani kwamba usalama wetu pekee, ili kuokoa roho zetu, ni kutomsujudia Mnyama na sanamu yake. Jambo hili liko mbele yetu na kila mtu atatakiwa kufanya uchaguzi, kwamba amsujudie Mungu aliyeziumba mbingu na nchi na bahari na vyote vilivyomo kwa kuzishika amri zake (soma Ufunuo 14:6-7) au amsujudie mnyama na sanamu yake, ambako kwa kweli ni kumsujudia Shetani mwenyewe (soma Ufunuo 13:2.) Katika Ufunuo 13:11-18 inaongezea juu ya ufalme (utawala) utakaolazimisha dunia na wote waliomo kumsujudia Rumi lakini Ufunuo 17:12-18 inaongezea kufunua jambo hilo zaidi kwa kuonyesha kuwa licha ya ufalme au utawala mmoja utakaolazimisha ibada hii iliyo kinyume na Mungu, tawala zingine pia duniani (wafalme kumi) wataungana katika kutekeleza jambo hilo. Hivyo tunachojifunza hapa ni kuwa tawala zote za dunia zitaungana kulazimisha ibada kwa kufuata mwongozo wa Kanisa la Rumi (soma Ufunuo 16:13-14.) Wafalme hawa watapokea mamlaka pamoja na yule mnyama, yaani kutakuwa na muungano maalum kati ya Kanisa la Rumi na mataifa ya dunia hii kutimiza jambo hili. Kumbuka kuwa Rumi inamafundisho yake yaliyo kinyume kabisa na neno la Mungu.

- "Sanamu ya Mnyama" – Sanamu ni mfano wa kitu halisi. Kama Mnyama ni mamlaka ya Kanisa la Rumi (RC), sanamu yake ni mamlaka ipi? Mamlaka nyingine ya Kikristo iliyofuata baadhi ya mafundisho ya Rumi na hivyo kuchanganya neno la Mungu na mapokeo, ni Uprotestanti. Hivyo sanamu ya Mnyama ni UPROTESTANTI ULIOASI, ambao ijapokuwa unadai umejitenga na Kanisa la Rumi, lakini mafundisho yao makuu ni yaleyale ya Rumi, na leo makanisa hayo yako mbioni kurudi kwa mama yao – KUUNGANA (soma Ufunuo 17:5.)

- "Chapa Katika Kipaji cha Uso" – Akili ndiyo sehemu muhimu inayohusika katika ufahamu na uamuzi mtu unaoweza kuufanya (soma 2 Wakorinto 5:13, Waefeso 5:15-17.) Hivyo, kukubaliana na mafundisho na mfumo utakaowekwa na serikali za dunia zikishirikiana na Kanisa la Rumi, ndiko kupokea chapa katika kipaji cha uso. *Jambo la muhimu kukumbuka ni kuwa kimsingi imani ya Kirumi inayakubali mambo yote ya msingi yaliyomo katika dini nyingine, na hivyo kwa msingi huo, hata dini nyingine zitakubaliana na mpango huu. (Je, hii ni kweli?)*

- “Chapa Mkononi” – Mikono yetu ndiyo viungo vikuu vya utendaji, kwa maana ya kutekeleza kazi. Ijapokuwa mwili mzima unahusishwa katika kazi, lakini mikono yetu ndio hasa hufanya sehemu kubwa kivitendo. Hivyo kupokea chapa ya Mnyama katika mkono ni kutekeleza kivitendo maamuzi au maelekezo yatakayotutaka tumsujudie Mnyama kwa kuiheshimu Jumapili kama siku ya Bwana.

Katika Ufunuo 13:8 inasema, “Na watu wote wakaao juu ya nchi watamsujudu, kila ambaye jina lake halikuandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwanakondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia.” Maandiko yako wazi kuwa wale ambao hawatamsujudu Mnyama ni wale ambao majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwanakondoo. Lakini je, ishara ya kuonyesha kuwa mtu anamsujudu Mnyama (Rumi) itakuwa nini? Ishara ya alama hiyo ni kuiheshimu Jumapili kama siku ya Bwana. Tulitangulia kujifunza kuwa Mungu Muumbaji anasema Sabato ndiyo ishara kati yake na watu wake ya kuwa yeye ndiye Mungu wao (soma Ezekieli 20:12,20) na Sabato ni Jumamosi. Lakini kwa sababu yule Mnyama alipokea mamlaka toka kwa joka ambaye ni Shetani na ambaye ameendelea kupingana na Mungu tangu alipoasi, yeye naye aliweka siku inayoonyesha kuwa na yeye (Shetani) anaabudiwa au kusujudiwa, na siku hiyo ndiyo Jumapili (soma Mathayo 15:8-9 na Ufunuo 13:3-4.) Kwa nini, ndugu, usichague kusimama upande wa Bwana kwa kuzitunza amri zake na kuishika Sabato yake? Je, jina lako linawezaje kuandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwanakondoo? Tafakari kisa hiki. Wakati Waisraeli walipozidi kumwasi Bwana jwangwani, Mungu alimwambia Musa kuwa atawaangamiza Waisraeli halafu atamfanya yeye (Musa) kuwa taifa kuu (soma Kutoka 32:9-11.) Lakini Musa akamsihi Bwana na kusema, “Walakini sasa ikiwa utawasamehe dhambi yao na kama sivyo unifute, nakusihi, katika kitabu chako ulichokiandika” (Kutoka 32:32.) Lakini “Bwana akamwambia Musa, mtu yeyote aliyenitenda dhambi ndiye nitakayemfuta katika kitabu changu….” (fungu la 33.) Kwa hiyo mtu anayeandikwa katika kitabu cha uzima cha Mungu ni yule aliyesamehewa dhambi (amekiri, ameungama na kuziacha) na amehesabiwa haki. Na kama tulivyotangulia kujifunza, mdhambi anasamehewa au anahesabiwa haki pale anapomkiri na kumwamini Bwana Yesu na hapo ndipo jina lake huandikwa katika kitabu cha uzima (soma Matendo 2:38-39 na Warumi 3:21-26.) Kwa kuwa Kristo anapopokelewa moyoni anatupatia uwazo wa kumtii Mungu kwa kuzishika amri zake, basi yeyote atakayempokea Yesu ataonyesha utii kwa amri hizo. Hivyo utii mkamilifu kwa amri za Mungu utakuwa ngao dhidi ya hatari ya kumsujudia Mnyama na sanamu yake.

Mungu wetu wa upendo ametufunulia mambo haya wazi. Kwa nini tupotee? Hebu mchague Yesu leo na uamue kuishi sawasawa na amri zake ili jina lako liwe katika kitabu cha uzima, usije ukamsujudu Mnyama badala ya kumsujudia Mungu.

- “Kunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu” - Ni hukumu ya kutisha, au adhabu kali watakayopata wale wote watakaomsujudu yule mnyama (Roma). Ufunuo 15:1;16:1-21. Wote watakaokataa kuupokea ukweli, watakuwa wamechagua adhabu hiyo.

- “Isiyochanganywa na maji” - Maana yake isiyo na huruma (soma Yakobo 2:13).

- “Kuteswa kwa moto na kiberíti” - Adhabu katika ziwa la moto (soma Ufunuo 20:10-15).

Wakati tunaelezwa juu ya wale watakaomsujudu mnyama na sanamu yake, tunaelezwa pia juu ya watakatifu wa Mungu katika saa hii ya mwisho ambao neno la Mungu linasema watatambulikana kwa kuzishika amri za Mungu na kuwa na imani ya Yesu, ishara kuu itakayowatambulisha ni kuitakasa na kuitunza Sabato ya siku ya saba ya juma, yaani Jumamosi. Kumbuka Sabato ndiyo ishara ya Mungu wa kweli aliye muumbaji.

Mpendwa msomaji, sasa tunasimama ukingoni kabisa mwa wakati wa kufungwa kwa rehema na historia ya dunia hii. Ukweli wa neno la Mungu umefunuliwa wazi kwetu, kwa nini tusichague kuokolewa sasa kabla hatujachelewa milele (soma 2 Kor. 6:2)? Usije ukadharau maneno haya kama jambo dogo tu. Pima kila kitu kwa nuru ya neno la Mungu. Kabla ya kufika mwisho, napenda nikukumbushe visa viwili vya pekee ili kukusaidia - Kisa cha kwanza ni uasi wa Adamu na Hawa. Unajua kwa akili yetu, kula tunda ni jambo dogo sana, lakini je, matokeo haya mabaya na ya kutisha yaliyoenea duniani leo unajua ni kutokana na hili lililoonekana dogo tu? Kisa cha pili ni wakati Sodoma na Gomora ilipoangamizwa kwa moto. Baada ya Lutu na mkewe na binti zao wawili

kutolewa nje ya mji, walipewa sharti la kutotazama nyuma na kuwa yeyote ambaye angetazama nyuma angeangamizwa pamoja na miji ile. Mke wa Lutu aligeuka nyuma na akawa nguzo ya chumvi (soma Mwanzo 19:17,23-26). Kugeuka nyuma tu!! Hivyo mpendwa, hebu kwa neema ya Mungu, iliyofunuliwa kweli kwa njia ya Kristo Yesu Bwana wetu, tuzingatie ujumbe huu, tutubu, tufungue mioyo yetu na kuupokea ukweli wa neno la Mungu na kumpokea Yesu mioyoni ili awe Bwana na mwokozi wa maisha yetu binafsi, ili tupate kuokolewa tusipotee na dunia. Wito wa Mungu wa mwisho unasema "Tokeni kwake, enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake" (Ufunuo 18:4). Tokeni Babeli.

Mungu anakuita utoke Babeli ili upone. Je, utaitikia wito huo wa rehema? Yesu yu karibu mlangoni kuja kuchukua wateule wake (soma Yohana 14:1-3).

Huu utakuwa ndio mwisho wa pambano au vita vile vilivyoanzia kule mbinguni kati ya Mikaeli (Yesu) na malaika zake na Ibilisi na malaika zake, kwa hiyo, kumbuka kuwa uamuzi wowote utakaoufanya utakuwa unakuweka upande wa mmoja kati ya hao majemedari wawili - Yesu au Shetani.

Lakini maandiko matakatifu yanasema kwamba Yesu aliishashinda vita kwa ajili yetu, na wote watakaomwamini atawapatia ushindi. Mungu akubariki ili umchague Yesu leo. Injili hii (habari njema ya ufalme) inapohubiriwa sasa, kila mtu anafanya uamuzi, kwa uzima (Yesu) au mauti (Shetani), na kila mtu atakapokuwa amekwishachagua ni upande gani atakayosimama, Bwana Yesu atarudi mara ya pili, na sasa hayuko mbali (soma Ufunuo 22:12). **Anakuja upesi.**

M W I S H O